CHUO KIKUU CHA NAIROBI

KITIVO CHA SANAA

IDARA YA KISWAHILI

# SAJILI YA SHERIA: MTAZAMO WA VITENDO USEMI

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika idara ya Kiswahili, chuo kikuu cha Nairobi.

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine kile kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

Sahihi ______________________________ Tarehe 01/03/2022.____

LUCY N GATUNE

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishiwa kwa lengo la kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi idara ya Kiswahili.

Sahihi ______________________________Tarehe 07-03-2022____

PROF IRIBE MWANGI

(Msimamizi)

Sahihi______________________________Tarehe 09/3/2022

DR AYUB MUKHWANA

(Msimamizi)

# TABARUKU

Ningependa kuitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa Jane Wangari na marehemu Francis Gatune kwa kunifungulia milango ya elimu hadi ngazi ya uzamili. Mlihakikisha kuwa nimepata msingi dhabiti wa masomo, mkajinyima ili nisome. Imani yenu kwangu imeniwezesha kufika kiwango cha uzamili.

Kwa babangu ambaye hakuishi kuona matunda ya kazi yake, nina imani kwamba unafurahi unaponitazama uwinguni ulipo. Kwa mamangu mpenzi, asante kwa maombezi yako na wosia wako.

Namtabarukia dadangu felister icharia kwa mchango wake katika safari hii. Asante kwa kunipa moyo na kuwa mwanga katika maisha yangu. Pengine bila mchango wako singeweza kukabiri changamoto nilizopata katika safari hii. Mola akubariki.

# SHUKRANI

Namshukuru Mola kwa kuniwezesha kufika hatima ya safari hii. Ni Safari ambayo imekuwa na changamoto si haba lakini kwa uwezo na neema zake Maulana nimeweza kufika kikomo. Namshukuru Mola kwa kunijalia afya katika kipindi hiki cha shahada ya uzamili, tuliabiri gari hili tukiwa wengi, ila si wote wameweza kukamilisha malengo yao.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Prof Iribe Mwangi na Dkt Ayub Mukhwana.Walinielekeza na kuniongoza ifaavyo. Nawashuru kwa mawaidha, busara, na maelekezo yao ya kitaaluma katika tasnifu hii. Walinipa muda wao kila nilipowahitaji. Katu sipuuzi changamoto ambazo walinipa, kwamba si kupita mtihani tu bali napaswa kuelewa kikamilifu jambo ambalo ninalifanya. Nyakati zingine haikuwa rahisi, lakini walinikumbusha kuwa lazima nizame kikamilifu katika uzamili. Mwongozo wao katika kazi hii ni jambo ambalo litanifanya kuwa mdeni wao milele.  Hakika, mmekuwa nyota ingaayo maishani mwangu. Mungu awabariki na awazindishie hekima maishani.

Nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili chuo kikuu cha Nairobi. Shukrani zangu ziwaendee Dkt Prisca Jerono, Dkt Mbuthia, Dkt Mweri, Prof Habwe, Prof Timamy, Dkt Ombogi, Dkt Zanja na Prof Kinene wa Mutiso. Nawashukuru kwa kunipa msingi na maelekezo katika usomi wangu chuoni. Maelekezo yenu yalinipa mwongozo katika safari hii. Mchango wenu umeniwezesha kutimiza malengo yangu ya kukamilisha shahada ya uzamili.

Namshukuru msajili wa mahakama kwa kunipa kibali cha kufanya utafiti katika mahakama ya Milimani. Tasnifu hii haingekamilika bila kibali hiki pamoja na mchango wa majaji na mawakiri waliyotafitiwa katika mahakama ya Milimani. Mchango wao uliniwezesha kupata data ya uchanganuzi. Mola awabariki.

Safari hii tuliabiri pamoja na wanafunzi ambao tulihimizana. Nawashuru: Dan, Jomo, Dorcas, Dekens, John, Nicodemus, Ruth, Anne, Violet, Agnes na Rehema. Tulifaana katika kila hali ya masomo yetu. Uvumilivu umetuwezesha kufika umbali huu. Mola awabariki na awazidishie darubini maishani, muweze kufika upeo wa masomo na wa nyanja zingine za maisha.

Nawashukuru marafiki wote wa nia njema. Siwezi kuwashukuru wote ila baadhi: Salome, Jael, Anne, Jeniffer na Peter. Asanteni kwa kunitia moyo na kunihimiza. Mchango wenu kwangu uliniwezesha kukabiri changamoto nilizopatana nazo.

Mwisho, nawashukuru ndungu zangu: Felister, Joyce, Joseph na Johnstone. Mlinihimiza na kuniombea katika safari hii.  Mmekuwa mhimili mkubwa katika masomo yangu na maisha yangu kwa jumla. Mungu awabariki na awakithie mahitaji yenu.

## IKISIRI

Utafiti huu unalenga kuchunguza sajili ya sheria kwa mtazamo wa vitendo usemi. Sajili hii itachunguzwa kwa mujibu wa nadharia ya vitendo usemi. Kazi katika tasnifu hii imepangwa katika sura tano, ambapo sura ya kwanza tutaangazia utangulizi kuhusu mada ya utafiti. Sura hii itatuelekeza kuhusu kile kitakachotafitiwa katika kazi hii. Sura ya pili tutachunguza kategoria za vitendo usemi katika sheria. Sura ya tatu itahusu umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria. Katika sura ya nne tutachunguza mchango wa vitendo usemi kwa sajili ya sheria. Sura ya tano ni muhktasari, mahitimisho na mapendekezo. Data hii itawasilishwa kwa njia ya maelezo, mifano na mijadala katika sura hizi.

Matumiziya vitendo usemi katika diskosi ya sheria yametuwezesha kubaini kuwa, lugha ya sheria ni lugha tendaji kwani kila usemi katika sheria una jukumu tekelezi. Tumebainisha kuwa vitendo usemi hutumiwa na wanasheria ili kufanikisha malengo yao kikazi. Kwa kufanya hivi, kategoria mbali mbali za vitendo usemi hutumiwa na wanasheria. Utafiti huu umebainisha kuwa asilimia kubwa ya vitendo usemi hutumiwa na mawakili ikiliganishwa na mahakimu. Utafiti huu umebaini kuwa vitendo usemi huwa na umuhimu kwa matapo haya mawili ya wanasheria. Yaani, mawakili na mahakimu. Matumizi ya vitendo usemi huwawezesha kufanikisha kazi zao kisheria.

## VIFUPISHO VYA MANENO

J : Jaji

KM : Kiongozi wa mashtaka

M : Mshukiwa

OWP : Ofisa wa upelelezi

SH : Shahidi

W : Wakili

V : Vitendo

**YALIYOMO**

UNGAMO……………………………………………………………………………………ii

TABARUKU…………………………………………………………………………………iii

SHUKRANI………………………………………………………………………………… iv

IKISIRI………………………………………………………………………………………vi

VIFUPISHO……………………………………………………………………………...vii

YALIYOMO……………………………………………………………………………...vii

**SURA YA KWANZA…………………………………………………………………1**

1.1.USULI WA MADA………………………………………………………………......1
1.2.TATIZO LA UTAFITI………………………………………………………….......3
1.3.MASWALI YA UTAFITI…………………………………………………………..3
1.4.MALENGO YA UTAFITI…………………………………………………………..3
1.5.SABABU ZA KUCHAGUA MADA…………………………………………….....4
1.6.UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI……………………………………………......6
1.7.YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA………………………………....................7
1.8.NADHARIA…………………………………………………………………………10
1.9.MBINU ZA UTAFITI……………………………………………………………….17
1.9.1. ENEO LA UTAFITI……………………………………………………………….17
1.9.2. SAMPULI…………………………………………………………………………….17
1.9.3. MBINU ZA KUKUSANYA DATA…………………………………………………18
1.9.4. MBEKO KATIKA UTAFITI…………………………………………………………19
1.9.5. UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA…………………………………...19

**SURA YA PILI……………………………………………………………………………….21**

2.0. KATEGORIA ZA VITENDO USEMI KATIKA SHERIA……………………………...21

2.2. UCHANGANUZI WA DATA NA MIJADALA…………………………………..…21

2.2.1. VITENDO ELEKEZI……………………………………………………………......22

2.2.2. VITENDO VYA AHADI……………………………………………………………24

2.2.3. VITENDO VYA KUTAARIFISHA……………………………………………………26

2.2.4. VITENDO VYA UAMUZI…………………………………………………………....28

2.2.5. VITENDO VIELEZI…………………………………………………………….......30

2.3 MATOKEO YA UTAFITI KUHUSU VITENDO USEMI……………………………….31

2.4. HITIMISHO……………………………………………………………………………31

**SURA YA TATU…………………………………………………………………………..35**

3.1 UMUHIMU WA VITENDO USEMI KWA WANASHERIA……………………………35

3.2. MATOKEO YA UTAFITI KUHUSU UMUHIMU WA VITENDO USEMI KWA WANASHERIA……………………………………………………………………….35

3.3. UCHANGANUZI WA DATA NA MIJADALA KUHUSU UMUHIMU WA VITENDO USEMI……………………………………………………………………………….39

3.3.1. KUAMRISHA…………………………………………………………………...39

3.3.2. KUTOA UFAFANUZI………………………………………………………….40

3.3.3. KUHOJI…………………………………………………………………………….42

3.3.4. KUTIA MOYO………………………………………………………………….43

3.3.5. KUARIFU…………………………………………………………………………44

3.3.6. KUTANGAZA…………………………………………………………………...44

3.4. HITIMISHO…………………………………………………………………………...45

**SURA YA NNE…………………………………………………………………………47**

4.1. MCHANGO WA VITENDO USEMI KWA SAJILI YA SHERIA………………………47

4.2. MATOKEO KUHUSU UMUHIMUWA VITENDO USEMI KATIKA SHERIA………………………………………………………………………………47

4.2.1. UCHUNGUZI AU UDADISI…………………………………………………48

4.2.2. KUDHIBITI MAHUSIANO YA WATU KATIKA JAMII…………………………...51

4.2.3. UAMUZI WA MAHAKAMA……………………………………………………56

4.2.4. KUHOJI NA KUTOA UFAFANUZI……………………………………………58

4.2.5. KUTAARIFISHA AU KUARIFU………………………………………………62

4.3. HITIMISHO……………………………………………………………………………66

**SURA YA TANO…………………………………………………………………………67**

5.1. MUHTASARI, MAHITIMISHO, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO……………...67

5.2. MUHTASARI…………………………………………………………………….67
5.3. MAHITIMISHO………………………………………………………………….69
5.4. CHANGAMOTO ZA UTAFITI………………………………………………….70
5.5. MAPENDEKEZO…………………………………………………………….....70
**MAREJELEO………………………………………………………………………....72**
**DATA YA UCHANGANUZI……………………………………………………………74**
**VIAMBATISHO……………………………………………………………………………….82**

## SURA YA KWANZA

### 1.0.USULI WA MADA

Utafiti huu unahusu sajili ya sheria. Ni utafiti ambao umejikita katika isimu jamii ili kuchunguza sajili ya sheria kwa mtazamo wa vitendo usemi. Uchunguzi wetu utaongozwa na nadharia ya vitendo usemi katika kuchunguza utendaji wa lugha katika diskosi ya sheria. Waithira (2014), anaeleza kuwa, lugha ya sheria hutambulishwa na hali ya matumizi ya lugha sanifu, lugha tendaji na lugha ya kiufundi. Ufundi huu hutokana na sababu kuwa sheria huwa na jukumu la kimsingi la kudhibiti tabia za binadamu. Kutokana na misingi hii, nadharia ya vitendo usemi itatuongoza katika utafiti wetu. Uteuzi wa nadharia hii ulitokana na ufaafu wake kuhusu masuala yatakayochunguzwa.

Kwa mujibu wa Danet (1980), sajili ya sheria huhusisha matumizi ya vitendo usemi. Danet anaeleza kuwa, vitendo usemi vya uamuzi na elekezi hutumika sana katika sheria. Vitendo elekezi hutumika na wanasheria katika kupata ushahidi. Aidha, majaji hutumia vitendo vya uamuzi katika kutekeleza haki katika jamii. Vitendo usemi katika muktadha wa sheria huwa na mchango mkubwa kwa wanasheria. Wanasheria hutumia lugha kuunda sheria na kusuluhisha migogoro katika jamii. Kundi hili huwa ni kiungo muhimu cha kutekeleza haki. Lugha ambayo hutumiwa na kundi hili katika utekelezaji wa kazi zao huwa ni lugha sanifu na ya kiufundi jambo ambalo huwatofautisha na makundi mengine ya kijamii. Katika kuchunguza sajili ya sheria kwa mtazamo wa vitendo usemi, lugha ya mawakili na majaji katika mawasiliano rasmi itachunguzwa ili kuweza kubainisha kategoria za vitendo usemi zinazojitokeza katika sajili ya sheria.

Lugha ni muhimu sana katika mfumo wa kisheria. Sheria hupitishwa kwa kutumia lugha. Kiguru (2014), akimnukuu Fletcher (2003), anaeleza kwamba sheria ni uwanja wa vitendo usemi, kwani ni katika sheria pekee ambapo lugha huonekana kwa uwazi ikifanya vitendo ukiliganisha na nyanja zingine zote. Katika jamii, sheria hufasiriwa na kutekelezwa kwa kutumia lugha. Kwa hivyo, lugha huwa ni chombo cha kufanikisha mchakato wa kisheria. Danet (1980), anaeleza kuwa sheria

haingekuwepo bila uwepo wa lugha. Kuligana naye, sheria ina majukumu mawili ya kimsingi katika jamii:

(i) Kuhakikisha kuna usawa katika mahusiano ya kibinadamu.
(ii) Kurejesha amani katika jamii wakati amani imevurugika.

Jukumu la kwanza linahusu uundaji na mpangilio wa kanuni ambazo hutawala tabia za jamii. Kimsingi hii ni sheria ambayo imeandikwa na inayoelekeza binadamu katika mahusiano yake na wengine. Jukumu la pili linahusu kufanikishwa kwa sheria kupitia mfumo wa mahakama, ambapo haki hupatikana. Wanasheria sharti watumie lugha katika maigiliano yao kazini. Mwingiliano huu ndio utakuwa msingi wa utafiti wetu katika kuchunguza umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria. Muktadha ni kipengele muhimu katika mawasiliano kwa sababu maana hutokana na muktadha, (Sharpe 2007). Kwa hivyo, muktadha huwa na umuhimu mkubwa katika kuelewa maana ya maneno yanayotumiwa katika lugha mbalimbali. Katika muktadha wa sheria lugha inaweza kuleta mabadiliko katika jamii. Mabadiliko haya yanaweza kuwa chanya au hasi kutegemea uamuzi ambao hufanywa na hakimu. Matumizi ya lugha ya sheria huwa na ushawishi mkubwa kimazungumzo na huchangia sana kuleta mabadiliko haya. Wanasheria hutumia mikakati ya kipragmatiki kama vile vitendo usemi katika muktadha wa sheria. Mikakati hii huwa na mchango mkubwa katika diskosi ya sheria kwani uamuzi unaofanywa na jaji hutegemea kwa kiwango kikubwa jinsi lugha imetumika katika mchakato mzima wa kesi. (Kiguru 2014).

Kwa mujibu wa Croetteli (2002), mahakama ni mahali ambapo maelezo hurudiwarudiwa. Sababu kuu ya urudiaji huu ni haja ya kujaribu kuangalia ubora wa kesi zilizowasilishwa. Maelezo haya hayarudiwi tu kabla ya kesi bali hudhihirika katika mchakato wote wa kesi. Anaendelea kusema kuwa, katika muktadha wa sheria, mojawapo ya sauti ambazo husikika sana mahakamani ni sauti ya wakili. Hali hii hutokana na hadhi yake na ushawishi mkubwa aliyonao katika kesi iliyowasilishwa. Wakili hufanikisha kazi yake kupitia maswali na majibu ambayo huulizwa mashahidi au washukiwa. Maswali haya huwezesha ujenzi wa kesi katika misingi ya maelezo yaliyowasiliswa kuhusiana na kesi husika. Kiguru (2014), akimnukuu Farinde (2009), anaeleza kuwa maswali ndio vitendo usemi vikuu katika mahakama na wanasheria huyatumia kama njia ya

kudhibiti yale yanayosemwa na mashahidi na washukiwa. Woodbury (1984), anasema kuwa maswali ambayo huulizwa kotini huweza kuainishwa katika kategoria mbali mbali. Kuligana naye maswali haya yanaweza kuwa ya kijumla, maswali mbadala, maswali ya ndio au la na yanayohusu matangazo. Kwa kuchanganua maswali haya, tutaweza kuchanganua vitendo usemi mbalimbali kama vinavyotumika mahakamani. Aidha, uchanaganuzi wa lugha kupitia maswali haya utatuwezesha kuonyesha umuhimu wa vitendo usemi katika lugha ya sheria.

## 1.1.TATIZO LA UTAFITI

Utafiti huu unalenga kuchunguza lugha ya sheria kwa mtazamo wa vitendo usemi. Kategoria za vitendo usemi zijitokezazo katika sajili ya sheria zitabainishwa na umuhimu wa vitendo hivi katika sajili ya sheria utaelezwa.

Ingawa sajili ya sheria ni muhimu katika jamii, utafiti wa kina unaolenga matumizi ya vitendo usemi katika lugha ya sheria haujafanywa kwa kina ili kuweza kubainisha jinsi lugha ya sheria ni lugha tendaji. Wasomi kama vile Danet (1980, 1985), Eades (2000), Croetteli (2002) na Mathooko (2007) wameandika kuhusu lugha ya sheria hasa sifa bainifu za lugha hii. Hata hivyo, utafiti huu unachukua mtazamo tofauti wa isimu jamii, kwani sajili ya sheria itachunguzwa kwa kutumia mtazamo wa kipragmatiki ambao ni vitendo usemi. Tutachunguza jinsi wanasheria hutumia vitendo usemi katika muktadha rasmi wa kazi zao. Katika utafiti huu, tutachunguza lugha ya sheria kama lugha tendaji, jambo ambalo hufanya lugha hii kuwa na athari chanya au hasi katika jamii. Ni kutokana na pengo hili la kitaaluma katika sajili hii, ambapo utafiti huu unalenga kuchunguza utendaji wa lugha ya sheria kwani kila usemi katika sheria una jukumu tekelezi.

## 1.2.**MASWALI YA UTAFITI**

Maswali yafuatayo yatatuongoza katika utafiti wetu**.**

i. Je, ni kategoria zipi za vitendo usemi zijitokezazo katika sajili ya sheria.

ii. Je, matumizi ya vitendo usemi katika sajili ya sheria yana umuhimu wowote kwa wanasheria?

iii. Je, mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria ni upi?

## 1.4. MALENGO YA UTAFITI

Katika kuchunguza sajili ya sheria, malengo yafuatayo yatatuongoza na kutuwekea msingi wa kuchanganua matumizi ya vitendo usemi katika lugha ya sheria.[i] Malengo haya ni kama yafuatayo:

i. Kuonyesha kategoria za vitendo usemi katika sajili ya sheria.

ii. Kubainisha umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria.

iii. Kutathmini mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria.

## 1.5. SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Sheria ni kiungo muhimu katika jamii yoyote ile. Upo uhusiano mkubwa kati ya sheria na jamii, kwani sheria huundwa na kutekelezwa kwa madhumuni ya kufikia malengo fulani katika jamii. Sheria ina jukumu kubwa la kuleta amani na kuongoza jamii kwa njia zifaazo. Ukiukaji wa sheria husababisha adhabu fulani katika jamii. Aidha, mabadiliko mengi ambayo hufanyika katika jamii hufikiwa kwa kutumia sheria kama kichocheo cha kuleta mabadiliko katika jamii yoyote ile. Utafiti huu umejikita katika isimu jamii, Yatakayochunguzwa yanahusu uhusiano wa lugha na jamii. Kwa vile lugha ya sheria ni muhimu katika kuleta utagamano wa jamii, utafiti huu una

uwezo mkubwa wa kuendeleza isimujamii na vilevile kuonyesha upekee wa matumizi ya vitendo usemi katika muktadha wa kisheria.

Wanaisimu na wanasheria kwa jumla wametafitia sana kuhusu uhusianao uliopo baina ya lugha na sheria. Wasomi kama vile Danet (1980), Eades (2000), na Croetteli (2002), wametoa mchango mkubwa wa kiusomi katika kueleza jinsi lugha inavyotumika katika sheria. Mchango wao ulijikita sana katika sifa bainifu za lugha ya sheria na umuhimu wa lugha ya sheria. Hata hivyo, utafiti huu unalenga kuchunguza sajili ya sheria kwa kutumia mtazamo wa kipragmatiki, ambao ni matumizi ya vitendo usemi katika lugha ya sheria kwa kujikita katika muktadha wa Kiswahili. Kwa sababu hii, utafiti huu ni muhimu kwani utatoa uchanganuzi wa kina wa lugha ya sheria kama lugha tendaji. Aidha, dhima ya vitendo usemi katika muktadha wa kisheria itajadiliwa kwa kina na kubainishwa.

Fairclough (1989), anaeleza lugha kama chombo chenye uwezo mkubwa wa kudhibiti jamii na mamlaka. Uwezo huu hudhihirika wazi katika mfumo wa sheria na majukumu ya mahakama. Sheria ni kiungo muhimu katika jamii yoyote ile. Ili kufanikisha malengo yake, sheria hutumia lugha katika mawasiliano. Shabaha hizi katika sheria haziwezi kutimizwa bila uwepo wa mawakili na majaji, ngazi ambazo ni muhimu katika sheria hasa kutetea haki. Wanasheria hutumia lugha vitofauti na makundi mengine ya kijamii. Upekee huu katika matumizi ya lugha hubainisha sajili ya sheria na kuitofautisha na sajili zingine. Lugha ya sheria huwa tendaji kwani usemi katika sheria unaweza kusababisha matokeo fulani katika jamii kutegemea aliyeusema. Kwa sababu hii, utafiti wetu utakitwa katika kundi hili la kijamii katika kutathmini jinsi lugha ya sheria ni lugha tendaji. Utafiti huu utatoa uchanganuzi wa kina kuhusu vitendo usemi ambavyo hutumika na wanasheria katika muktadha wa sheria. Pia, utaonyesha jinsi nadharia ya vitendo usemi inaweza kueleza mahusiano yaliyopo baina ya lugha na uhalisia, huku lugha ya Kiswahili katika mahakama ikirejelewa.

Utafiti huu utawafaa sana wasomi wa baadaye katika uelewa wao kuhusu matumizi ya vitendo usemi katika diskosi ya sheria. Vilevile, utatoa changamoto kwao, hasa wale ambao wangependa kufanya utafiti kuhusu sajili ya sheria kwa kutumia mitazamo mingine ya kipragmatiki.

## 1.6. UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Diskosi ya sheria ni pana mno, haiwezekani kijishughulisha na masuala yote yanayoshughulikiwa na sheria. Sheria hujumuisha matumizi ya lugha ya kimaandishi na ya kimazungumzo ambayo hutumika katika chunguzi za kesi mahakamani. Utafiti huu hata hivyo, umejifunga katika lugha ya kimazungumzo kwa sababu maswali ya utafiti kuhusu matumizi ya vitendo usemi katika lugha ya sheria yamekitwa katika lugha ya kimazungumzo.

Mfumo wa mahakama una vitengo vingi ambavyo hushughulikia kesi tofauti tofauti. Kuna vitengo ambavyo hushughulikia kesi za jinai, kesi za madai, kesi za watoto, kesi za ufisadi, miongoni mwa zingine. Utafiti huu utajikita katika kitengo kinachoshughulikia kesi za jinai. Tutajikita katika kitengo hiki pekee kwani, chunguzi kuhusu vitengo vingine vyote vitaleta changamoto hasa katika uchanganuzi wa data kutokana na wingi wa data hiyo.

Katika utafiti huu tutachunguza lugha ya sheria kwa kujikita katika mtazamo wa vitendo usemi. Tutachunguza namna wanasheria hutumia vitendo usemi katika mazingira rasmi ya kazi zao. Hatutajishughulisha na matumizi ya lugha ya wanasheria nje ya muktadha rasmi wa kazi zao. Mazungumo ya kundi hili mahakamani ndio yatakuwa msingi wa uchanganuzi wa data yetu. Utafiti huu utafanyika katika mahakama ya Milimani ambayo tumeteua kama kiwakilishi cha mahakama nyingine.

## 1.7. YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Watafiti kadha wametalii matumizi na umuhimu wa maswali yanayotumika katika mfumo wa sheria. Lyons (1977), alieleza tofauti kati ya maswali ya kudadisi na sentensi za kudadisi ambazo hutumiwa katika sheria. Kwa mujibu wake, maswali ni matamko ambayo hutumiwa na mzungumzaji wa lugha katika muktadha ili kutimiza jukumu fulani la kimawasiliano. Maoni haya ni sawia na ya Danet (1980), ambaye anaeleza kwamba, katika kesi maswali hutumika kama njia ya kupata taarifa na kudhibiti yanayosemwa. Anaeleza kuwa, maswali hutoa taarifa kuhusu suala linalochunguzwa. Maswali haya pia hudai majibu ambayo hudhibitisha taarifa iliyotolewa. Woodbury (1984), anasema kuwa maswali ambayo huulizwa mahakamani huweza kuainishwa katika kategoria mbalimbali. Anaeleza kuwa, maswali haya yanaweza kuwa ya kijumla, maswali mbadala, maswali ya ndio au la na yanayohusu matangazo. Mawazo ya wasomi hawa yanaendelezwa na wasomi kama vile Kiguru (2014). Kiguru akimnukuu Farinde (2009), anaeleza kuwa, maswali ndio vitendo usemi vikuu katika mahakama na wanasheria huyatumia kama njia ya kudhibiti yale yanayosemwa na mashahidi. Kazi za wasomi hawa zinahusiana na yale yatakayotafitiwa katika utafiti huu kwani, utafiti wetu unalenga kutalii sajili ya sheria kwa mtazamo wa vitendo usemi. Maswali yanayoulizwa katika mchakato wa mawasiliano baina ya wanasheria yatatumika kama msingi wa utafiti wetu ili kubaini kategoria za vitendo usemi katika sajili ya sheria. Maswali kati ya wanasheria, washtakiwa na vile vile mashahidi yatatumika kama msingi wa uchanganuzi data. Kwa kutumia maswali haya tutaweza kubaini ni kategoria zipi za vitendo usemi hutumika kwa wingi katika lugha ya sheria. Maswali ya udadisi, maswali ya kijumla, maswali ya ndio au la na maswali mbadala yatachanganuliwa na utendakazi wake kuelezwa. Maswali haya yatatuwezesha kubaini umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria. Vilevile, tutaweza kuchanganua jukumu tekelezi la lugha ya sheria kwani kila usemi katika sheria huwa ni tendaji.

Danet (1980), alichunguza lugha ya sheria na kuangalia majukumu ya kimsingi ya lugha hii. Kwa mujibu wa Danet, sheria ina majukumu mawili: Kuhakikisha kuna usawa katika mahusiano ya kibinadamu na kurejesha amani wakati amani imevurugika. Majukumu haya hufanikishwa kimaandishi na kimazungumzo kupitia mfumo wa mahakama. Wanasheria huwa ndio kiungo

muhimu cha kufanikisha majukumu haya. Eades (2000), alitalii jinsi mawakili hutumia maswali kama njia ya kudhibiti maelezo ya shahidi. Kazi yake ilibaini jinsi hadhi ya mawakili huathiri matokeo ya uamuzi kutokana na jinsi wao hutumia lugha yenye ufundi wa kiwango cha juu. Croetteli (2002), ana mawazo yanayoligana na haya, anaeleza kuwa katika mfumo wa mahakama wanasheria ni kiungo muhimu kwani, ubora wa kesi hutegemea wakili. Katika mchakato wa kesi, sauti ya wakili husikika sana. Wakili hufanikisha kazi yake kupitia maswali na majibu. Kazi za wasomi hawa zitatufaa sana kwani dhamira yetu ni kuchunguza sajili ya sheria. Aidha, msingi wa uchanganuzi wa data yetu utategemea maswali ambayo huulizwa na wanasheria. Tafiti hizi zitatufaa sana katika kuchunguza matumizi ya vitendo usemi katika sheria. Maswali yanayotumiwa na wanasheria yatatuwezesha kubaini jinsi wanasheria hutumia vitendo usemi kama mkakati wa lugha yao. Kufaulu kwa utendakazi wao hutegemea maswali ambayo huwa ndio msingi wa ujenzi wa kesi mahakamani. Kutokana na hali hii basi, tutaweza kubaini mchango wa vitendo usemi kwa mahakimu na mawakili. Maswali haya vilevile, yatatuwezesha kuchanganua mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria. Data ya utafiti huu itachanganuliwa kwa mujibu wa maswali haya. Hata hivyo, utafiti wao utatofautiana na wetu kwani sisi tutatalii utendaji wa lugha katika sajili hii. Mkondo wa utafiti wetu hautaegemea sana majukumu na sifa za sajili ya sheria, bali shabaha ya utafiti wetu ni kuchanganua lugha ya sheria kwa mtazamo wa vitendo usemi.

Wood (2012), katika utafiti wake 'courtroom discourse as a verbal performance' alibaini kuwa, diskosi ya mahakama ina upekee fulani kutokana na jinsi lugha hutumika. Katika kazi yake, alitalii utendaji wa maneno katika mahakama kwa kukita utafiti wake katika wahusika mbalimbali ambao hushiriki katika kesi. Wahusika waliochunguzwa ni kama vile majaji, mawakili, mashahidi, na washukiwa. Maingiliano kati ya wahusika hawa yalichunguzwa kwa misingi ya vitendo usemi. Wood alibaini kuwa, diskosi ya mahakama huwa na sifa za kipekee za kiisimu, ambazo huitofautisha na diskosi zingine. Tofauti hizi hujitokeza katika viwango vya sintaksia, semantiki na pragmatiki. Kiguru (2014), alitafiti diskosi ya mahakama nchini Kenya. Katika utafiti wake alitumia mtazamo unaoligana na wa Wood (2012). Kiguru (2014), katika kazi yake 'critical discourse analysis of language used in selected court of law in Kenya' alichunguza matumizi ya lugha miongoni mwa wahusika mbali mbali katika diskosi ya mahakama. Nadharia ya vitendo

usemi ilitumika katika kueleza matumizi ya lugha katika diskosi hii. Katika utafiti wake alijikita katika mikakati ya kipragmatiki ambayo hutumiwa na mawakili, viongozi wa mashtaka na washukiwa ambao huwa hawana wakili wakati wa kesi. Katika utafiti wake aliweza kubainisha kwamba, lugha ya mawakili huwa inaathiri mashahidi ambao hawana uelewa wa lugha ya kiufundi kama mawakili, jambo ambalo huweza kuathiri uamuzi wa mahakama. Tafiti hizi zitatufaa sana katika kubainisha matumizi ya vitendo usemi kama mkakati wa lugha ambao hutumiwa na wanasheria ili kufaulisha kazi zao. Mawakili na mahakimu watachunguzwa ili kubaini ni kundi lipi hutumia vitendo usemi kwa wingi na kwa nini. Vilevile, kategoria za vitendo usemi kama vinavyotumiwa na makundi haya vitachunguzwa kwani utafiti wetu unalenga sajili ya sheria kwa mtazamo wa vitendo usemi. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana na utafiti wetu. Utafiti wetu hauhusu uchunguzi kuhusu athari za lugha ya mawakili, na viongozi wa mashtaka kwa mashahidi bali unachunguza jinsi vitendo usemi hutumika katika lugha ya sheria. Kwa kufanya hivi, tutaweza kueleza mchango wa vitendo usemi katika sheria.

Waithera (2014), alitalii changamoto za kutafsiri matini za kisheria. Utafiti wake ulibaini kuwa, matatizo ya kutafsiri matini za kisheria yanawezatokana na ukosefu wa uliganifu wa kiistilahi. Ukosefu huu unaweza kuleta changamoto katika uwasilishaji wa maana. Utafiti huu utatusaidia katika kutafsiri matini za kisheria na vivile lugha ya sheria kama inavyotumiwa na wanasheria. Vilevile, utatuwezesha kuchanganua data ya utafiti ambayo msingi wake ni lugha ya sheria. Maana na istilahi za kisheria zitaeleweka kwani lugha ya sheria si wazi. Vilevile, utendakazi wa lugha katika sheria utaeleweka kwani kila usemi katika lugha ya sheria una jukumu tekelezi. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na wetu. Tafiti zetu zinachunguza utendaji wa lugha katika sajili ya sheria wala si changamoto za kutafsiri matini za kisheria. Utafiti kuhusu changamoto za kutafsiri matini za kisheria utatusaidia sana katika kubaini changamoto ambazo tunaweza kumbana nazo katika tafsiri za matini za kisheria.

Wambui (2015), alichunguza lugha katika sajili ya biashara kwa mtazamo wa kipragmatiki. Katika utafiti wake aliangalia lugha kimaandishi na kimazungumzo. Vilevile, alieleza utendaji wa lugha katika sajili ya biashara kwa mtazamo wa vitendo usemi.

Katika utafiti wake aliweza kubainisha jinsi vitendo usemi vinavyoweza kufanikisha mawasiliano katika matangazo ya biashara. Utafiti huu utatufaa sana katika kuchanganua matumizi ya vitendo usemi kama mkakati wa kimawasiliano katika diskosi ya sheria. Mahakimu na mawakili watachunguzwa jinsi wanavyotumia vitendo usemi kama mkakati wa lugha katika kazi zao. Mchango wa vitendo usemi kwa makundi haya utaelezwa ili kuonyesha jinsi vitendo usemi kama mkakati wa kimawasiliano husaidia matapo haya mawili ya kijamii kufaulisha kazi zao. Aidha, nadharia ya vitendo usemi itatumika kama msingi wa uchanganuzi wa utafiti wetu. Nadharia hii itatusaidia kubainisha jinsi vitendo usemi hufanikisha mawasiliano katika muktadha wa sheria. Hata hivyo, utafiti wetu utatofautiana na utafiti wake kwani sisi tutajikita katika uchunguzi wa lugha ya sheria kama lugha tendaji wala si sajili ya biashara.

## 1.8. NADHARIA

Utafiti huu utachunguza lugha ya sheria kama lugha tendaji. Kwa sababu hii, tutatumia nadharia ya vitendo usemi. Nadharia hii itatuongoza katika kuchunguza jinsi vitendo usemi vinavyotumika katika lugha ya sheria na vilevile itatuwezesha kubainisha umuhimu wa vitendo usemi katika diskosi ya sheria.

Vitendo usemi ni tamko ambalo hutekeleza majukumu katika lugha na mawasiliano. Mwasisi wa nadharia hii ni Austin (1962). Kwa mujibu wa Austin (1962), lugha yoyote ina majukumu mawili: jukumu elezi na jukumu tendaji. Majukumu haya ya lugha hutekelezwa kupitia vitendo usemi. Kuligana na Austin, vitendo usemi huainishwa kuwili, yaani vitendo wazi na vitendo fiche. Vitendo wazi ni vitendo ambavyo huashiria kitendo halisi kama vile kubaliki, kulaani ama kupongeza. Aidha, vitendo fiche ni vitendo ambavyo havitokei katika usemi, yaani havioonyeshi jinsi kitendo kimefanyika. Vitendo fiche ni vitendo ambavyo vinaweza kutendeka au visitendeke. Utafiti huu utajikita katika vitendo wazi kama vinavyotumika katika lugha ya sheria.

Kwa mujibu wa Austin (1962: 14-15), ili vitendo usemi vifanikiwe kutendeka ni sharti pawe na marsharti ya heri au fanaka. Yaani, lazima kitendo kitendwe kwa kufuata utaratibu unaofaa, lazima

kitendo kitendwe kuligana na desturi, na ni sharti kitendo hicho kitendwe na mtu afaaye. Austin (1962: 108), aliainisha vitendo usemi katika kategoria tatu kuu:

i. Vitendo vya lokusheni
ii. Vitendo vya ilokusheni
iii. Vitendo vya palokusheni.

Lokusheni ni vitendo unavyosema kwa kutumia ufasaha wa lugha. Vitendo hivi hutendwa kwa kusema lugha kwa mujibu wa sheria zake (Austin 1962: 95-96). Vitendo vya ilokusheni, ni vitendo vyote vinavyotokana na vitendo vya lokusheni. Kulalamika, kugombana, kuagiza, na kuteua ni mifano ya vitendo vya ilokusheni.

Palokusheni huwa ni vitendo ambavyo ni matokeo ya vitendo vya ilokusheni. Kama vile, kuteuliwa, kubalikiwa, kuolewa, kumbembelezeka na kuraika. Nadharia ya vitendo usemi inaweza kutambulishwa kwa mihimili mitatu ambayo ni: Lokusheni, ilokusheni na palokusheni. Kazi hii itajikita katika mhimili wa ilokusheni katika kuchunguza matumizi ya vitendo usemi katika diskosi ya sheria. Austin (1962), aliainisha vitendo usemi katika makundi matano: Vitendo fafanuzi, vitendo elekezi, vitendo vya ahadi, vitendo vya uamuzi na vitendo vya hisia.

Mawazo ya Austin yaliendelezwa na wasomi wa baadaye kama vile John Searle na Van derveken. Searle alichukua mtazamo wa philosophia ya lugha kuhusu vitendo usemi katika kufafanua na kueleza sifa za jumla kuhusu lugha. Searle (1979), aliipanga nadharia hii kama ifuatavyo.

i. Proposisheni
ii Ilokusheni
iii Palokusheni

Kwa mujibu wa Searle, kila tamko lina kibainishi chake. Vibainishi hivi hujumuisha mambo kadha kama vile: vitendo tendaji, mpangilio wa maneno katika sentensi, mkazo wa maneno, uakifishaji na dhamira. Kazi ya Searle hutofautiana na ya Austin katika vipengele mbalimbali. Kwanza, Austin alitofautisha vitendo vya lokusheni, ilokusheni na palokusheni ilhali Searle aliegemea

sana vitendo vya ilokusheni kama mhimili mkuu wa nadharia yake. Vilevile, aliongeza dhana ya preposisheni katika kazi yake. Searle alizungumzia pia suala la mielekeo inayofaa katika lugha.

Searle (1979:12-20), aliviainisha upya vitendo usemi vilivyoshughulikiwa na Austin (1962). Katika kazi yake, Searle alivipanga vitendo usemi katika makundi matano makuu kutegemea nguvu za ilokusheni. Makundi haya ni kama yafuatayo:

i. Vitendo vya kutaarifisha**.** Kundi hili humfunga msemaji kwenye ukweli wa tamko fulani. Hii ni kategoria ambayo huelezwa na vitendo usemi ambavyo hufafanua imani ya msemaji kuwa jambo ni kweli. Vitendo vya kutaarifisha ni kama vile, kutoa mapendekezo, malalamishi na kutoa madai. Mwelekeo unaofaa wa kundi hili ni wa neno kwa ulimwengu. Sifa nyingine kuhusu vitendo hivi ni kuwa, vitendo hivi huwa vinahusiana na shauku ya msemaji.

ii. Vitendo elekezi. Hivi ni vitendo ambavyo humfanya msikilizaji kutenda jambo. Vitendo usemi katika kundi hili hutumika katika kuuliza maswali, kutoa ushauri, kulalamika, kusihi, kuamrisha na kualika. Mwelekeo unaofaa wa vitendo hivi ni wa neno kwa ulimwengu. Muktadha wa preposisheni wa vitendo hivi ni kwamba, msikilizaji hutenda vitendo vya siku sijazo. (Searle 1979: 14).

iii. Vitendo vielezi**.** Hivi ni vitendo usemi ambavyo hudhihirika wakati msemaji huonyesha hali yake ya kisaikolojia. Vitendo hivi hueleza hisia za msemaji. (Searle 1979:15).

iv. Vitendo vya ahadi. Kundi hili hutumia lugha kutenda vitendo vya siku sijazo, kama vile tendo la kuahidi na Kula kiapo. Mwelekeo unaofaa wa vitendo hivi ni wa ulimwengu kwa ulimwengu. Muktadha wa preposisheni kuhusu vitendo hivi ni kwamba, msemaji hutenda vitendo vya siku sijazo.

v. Vitendo vya uamuzi**.** Kundi hili linajishughulisha na matamko ambayo yanabadili hali ya msikilizaji. Uamuzi hubadilisha hali ya mambo kwa kutamka au kutangaza jambo. Kufaulu kwa vitendo hivi hutegemea msemaji, lazima anayetekeleza kitendo kile awe na uwezo wa kufanya hivyo. Vitendo katika kundi hili huchukua mielekeo miwili, yaani mwelekeo wa neno kwa ulimwengu na mwelekeo wa ulimwengu kwa neno. Sifa inayotambulisha vitendo hivi ni tangazo. (Searle 1979:16).

Searle vilevile alizungumzia dhana kuhusu mielekeo inayofaa katika lugha. Kwa mujibu wa Searle mwelekeo unaofaa ni namna ambayo usemi huhusiana na vipengele katika lugha na ulimwengu. Kuligana naye kuna aina nne za mielekeo inayofaa katika lugha. Mielekeo hii ni:

i. Mwelekeo wa ulimwengu kwa ulimwengu - huu ni mwelekeo ambao usemi hujitosheleza kivyake katika hali iliyoko ya mambo katika muktadha wa matumizi. kwa mfano kauli ya ukweli hudhihirisha mwelekeo huu. Vitendo vya kutaarifisha na vya uamuzi hudhihirisha mwelekeo huu.

ii. Mwelekeo wa neno kwa ulimwengu - huu ni mwelekeo ambapo usemi hujitosheleza katika muktadha wa preposisheni katika vitendo vya ilokusheni. Vitendo elekezi hupatikana katika mwelekeo huu.

iii. Jozi za mwelekeo unaofaa- Hapa ni pale usemi hubadilishwa ili kujitosheleza katika muktadha wa preposisheni katika matamshi. Vitendo vya uamuzi huchukua mwelekeo huu

iv. Mwelekeo uliobatilika –katika mwelekeo huu hakuna swali la kuonyesha kufaulu kwa vitendo usemi kati ya muktadha fulani na mwingine. Kwa mujibu wa Searle, vitendo ambavyo msemaji hueleza hisia zake huchukua mwelekeo huu. Vitendo viagizi huchua mwelekeo huu.

Katika utafiti huu tutatumia mpangilio wa Searle kwani kategoria za vitendo usemi zilizoainishwa na Austin (1962) zina utata na zimeelezwa kwa ujumla. Katika mpangilio wa Austin, hakuna

kanuni ya kimsingi iliyotumika kuainisha makundi haya ya vitendo usemi. Kwa upande mwingine Searle (1979), aliviainisha upya vitendo usemi vilivyoshughulikiwa na Austin kutegemea nguvu za ilokusheni. Vilevile, alishughulikia dhana ya preposisheni katika kueleza vitendo usemi katika makundi haya. Katika utafiti wetu tutatumia nadharia ya vitendo usemi kuchunguza kategoria mabali mbali za vitendo usemi zinazotumika katika sajili ya sheria. Mtazamo wa Searle (1979), utatusaidia kubaini kategoria hizi kama zinavyotumika katika sajili ya sheria. Mchango wa kategoria za vitendo usemi katika lugha ya sheria utaelezwa kwa mujibu wa nadharia hii.

Utafiti wetu vilevile utajikita katika mhimili wa ilokusheni. Mhimili wa ilokusheni utatumika kueleza kategoria za vitendo usemi katika lugha ya sheria. Kwa kufanya hivi, tutabaini jinsi vitendo usemi hutumiwa na wanasheria kama mkakati wa lugha ili kufaulisha kazi zao. Athari za vitendo usemi vilevile zitabainishwa na kuelezwa. Diskosi ya sheria itachunguzwa huku maswali yakitumiwa kama msingi wa uchanganuzi wa data itakayochanganuliwa kwa mujibu wa nadharia ya vitendo usemi. Kupitia kwa maswali kati ya wanasheria, mashahidi na washtakiwa kategoria za vitendo usemi katika muktadha wa sheria zitabainika kama zinavyotumiwa na makundi haya mahakamani.

Searle na Van derveken (1985), wanaeleza dhana ya nguvu za ilokusheni. Kuligana nao, kuna aina mbalimbali za nguvu za ilokusheni, ambazo huelezwa kupitia kwa vipengele vifuatavyo:

i. Kiini cha ilokusheni

Sehemu kuu au kijenzi kikuu cha nguvu za ilokusheni huwa ni kiini chake. Kuligana na Searle (1975), kiini cha nguvu za ilokusheni ni yale msemaji hunuia kufanya na kufuata wakati wa utendaji wa tendo za ilokusheni. Kwa mfano:

a) Kiini cha madai ni kutoa madai fulani ya hali ya mambo kama ya ukweli katika utamkaji.
b) Kiini cha ilokusheni kuhusu msamaha ni kueleza msikilizaji masikitiko kuhusu hali ya mambo.

ii. Masharti ya preposisheni katika muktadha

Hivi ni vikwazo ambavyo huwekwa katika vitendo usemi na muktadha wa preposisheni. Kwa mfano, inakuwa vigumu kubashiri jambo ambalo tayari limetendeka. Vivyo hivyo, ni vigumu kuahidi kutenda au kufanya kitendo ambacho tayari kimetendeka. Iwapo kitendo hicho kitafanywa baada ya kutendeka, kitendo hicho kitakuwa hakina maana. Masharti mengine ya kufaulu kwa utendaji wa vitendo vya ilokusheni ni kuwa, msemaji hueleza preposisheni ambayo ni muktadha wa kitendo hiki na kuwa nafasi hiyo ya preposisheni hudhihirisha masharti ya muktadha wa preposisheni.

iii. Masharti ya maandalizi

Kila kitendo cha ilokusheni huwa na masharti ya maadalizi. Hii ni hali muhimu kwani msemaji huchukulia kwamba maandalizi ni muhimu katika matamshi wakati wa utendaji wa kitendo fulani katika muktadha. Kwa mfano:

a) Masharti ya maandalizi ya tendo la ahadi ni kuwa msemaji anaweza kuweka ahadi hiyo.
b) Masharti ya maandalizi kuhusu madai ni kuwa msemaji ana sababu za ukweli wa hali fulani ya madai hayo.
c) Masharti ya maandalizi kuhusu ombi ni kuwa msikilizaji ana uwezo wa kutimiza ombi hilo.

Hata hivyo, msemaji huenda akafaulu kuonyesha utendaji wa tendo fulani bila kuwa na sababu yoyote kuhusu ukweli wa tendo hilo. Kama vile, msemaji anaweza kuahidi kufanya jambo ambalo hawezi kufaulu kulifanya. Kwa mfano, mtu anapoahidi kwamba atazungumza na mtu aliyeaga. Ni dhahiri kwamba usemi huu hauna ukweli wowote lakini huenda msemaji akafaulu kuonyesha ukweli wa tendo hilo.

Kitendo cha ilokusheni ambacho kimefaulu lakini masharti ya matayarisho hayana mashiko huitwa ilokusheni yenye upungufu. Kwa hivyo, kila kitendo usemi kisicho na upungufu hufaulu lakini si kila kitendo usemi ambacho kimefaulu huwa hakina upungufu.

Iv. Masharti ya ukweli

Masharti haya huhakikisha kuwa kitendo usemi kinachotendwa huakisi imani, nia na hisia za msemaji. Masharti haya hudhihirika wakati msemaji hueleza hali fulani ya kisaikolojia inayooana na muktadha wa preposisheni. Katika hali hii msemaji hudhani kwamba aliyoyasema ni kweli. Kwa mfano, tendo la kusihi huwa na nguvu nyingi za masharti ya kweli ikiliganishwa na tendo la kuomba. Msemaji ambaye huahidi kufanya jambo hueleza nia yake ya kutenda jambo

hilo. Hata hivyo si lazima msemaji awe mkweli ili kitendo cha ilokusheni kifaulu. Uongo kwa upande mwingine huenda ukawa madai ambayo yanaweza kufaulu kama kitendo cha ilokusheni.

Nadharia ya vitendo usemi itatuwezesha kubainisha kuwa lugha ya sheria ni lugha tendaji. Usemi wa kisheria huwa na jukumu tendaji jambo ambalo linadhihirishwa kwa matumizi ya vitendo usemi katika takribani mchakato wote wa kimawasiliano katika diskosi ya sheria. Mawazo ya wataalamu hawa kuhusu nadharia ya vitendo usemi yatatusaidia sana katika uchunguzi wetu kuhusu nafasi ya vitendo usemi katika lugha ya sheria. Vile vile, mawazo yao yatakuwa ya umuhimu katika kueleza jinsi vitendo usemi hufanikisha mawasiliano katika diskosi ya sheria huku tukirejelea matumizi ya lugha ya sheria katika mahakama ya Milimani jijini Nairobi.

Utafiti huu una mchango mkubwa kwa nadharia ya vitendo usemi. Kupitia utafiti huu tumeweza kubaini mchango wa vitendo usemi kwa sajili ya sheria. Matumizi ya vitendo usemi katika lugha ya sheria huwa na umuhimu ufuatao kama ulivyobainika kutokana na utafiti wetu: uchunguzi au udadisi, kudhibiti mahusiano ya watu katika jamii, kutaarifisha na kutoa maamuzi mahakamani. Michango hii imebainika kupitia matumizi ya lugha kwa wanasheria. Aidha, tumebainisha kwamba vitendo usemi huwa ni mkakati wa lugha ambao hubainisha sajili ya sheria, kwani wanasheria hutumia mkakati huu kufaulisha kazi zao. Vile vile, tumeweza kubaini kuwa matumizi ya vitendo usemi katika lugha ya sheria hufanya lugha hii kuwa na jukumu tekelezi kwani kila usemi katika lugha ya sheria huwa na jukumu tendaji. Maelezo kuhusu mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria yameelezwa kwa kina katika sura ya nne.

## 1.9.MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ni utafiti fafanuzi. Kwa mujibu wa Kothari (2004), utafiti fafanuzi hufanywa ili kuonyesha sifa za mtu binafsi, kundi au hali. Utafiti wa aina hii hufanywa hasa katika masuala ya sayansi jamii. Mugenda (2008), anaeleza kuwa utafiti fafanuzi hutumika katika kuchunguza masuala ya kijamii na huwezesha mtafiti kutoa suluhu na mapendekezo kuhusu masuala

yaliyochunguzwa. Utafiti wetu unalenga kuchunguza sajili ya sheria kwa mtazamo wa vitendo usemi. Kategoria za vitendo usemi zinazojitokeza katika sajili ya sheria zitachunguzwa. Aidha, umuhimu wa matumizi ya vitendo usemi katika diskosi ya sheria utachunguzwa. Masuala haya yataweza kuchunguzwa vyema katika utafiti fafanuzi.

Utafiti huu ni wa nyanjani, kwa hivyo itatubidi kuzuru eneo la utafiti ambalo ni mahakama ya Milimani mjini Nairobi ili kukusanya data juu ya lugha ya sheria. Data hiyo itachanganuliwa baadaye kwa mujibu wa nadharia vitendo usemi.

### 1.9.1. ENEO LA UTAFITI

i

Utafiti huu utafanyika katika mahakama ya Milimani ambayo tumeiteua kama kiwakilishi cha mahakama nyingine. Uteuzi wa mahakama hii umetokana na sababu kuwa mahakama hii ni mahakama ya chini katika ngazi ya hakimu. Kiguru (2014), anaeleza kuwa kuligana na migawanyo ya kijiografia mahakama ya chini ndio nyingi sana na kwa hivyo idadi ya kesi zinazoshughulikiwa katika mahakama hizi huwa nyingi hususan katika mahakama ya ngazi ya hakimu. Mahakama ya Milimani hivyo basi, imeteuliwa kimaksudi kwa kuwa inashughulikia mseto wa kesi nyingi na kwa hivyo tutaweza kupata data ya kutosha katika utafiti wetu.

### 1.9.2. SAMPULI

Sampuli ni sehemu ndogo ya kundi nzima ambayo hutafitiwa kama kiwakilisha cha kundi nzima linalotafitiwa. Utafiti huu utatumia sampuli ya kimaksudi. Kothari (2004), anaeleza sampuli ya kimaksudi kama aina ya sampuli ambayo huhusisha uteuzi wa kundi la watu au vitu kama kiwakilishi cha kundi nzima. Anaendelea kusema kuwa sampuli ya kimaksudi hutumika wakati kundi au hali inayochunguzwa huwa ndogo na sifa zinazofahamika kuhusu kundi husika huchunguzwa kwa kina. Kutokana na misingi hii utafiti wetu utajikita katika sampuli ya kimaksudi. Katika utafiti huu mawakili na majaji watachunguzwa namna wanavyotumia lugha katika muktadha rasmi wa kazi zao. Lugha ya makundi haya itatuwezesha kubaini matumizi ya

vitendo usemi katika sajili ya sheria. Hali hii itatupa data inayohitajika kwa ajili ya utafiti wetu hasa tukirejelea malengo na maswali ya utafiti huu.

Mahakama hutoa orodha ya kesi ambazo zitasikizwa mahakamani na kutaja siku ambazo kesi hizo zitasikizwa. Hata hivyo, si lazima kesi hizo zisikizwe kama zilivyoratibiwa kwani zinaweza ahirishwa na kufanyika siku nyingine. Hali hii imesababisha uteuzi wa sampuli ya kimaksudi katika ukusanyaji wa data inayohitajika.

### 1.9.3. MBINU ZA KUKUSANYA DATA

Kwa kuwa huu ni utafiti wa nyanjani, mtafiti atahudhuria kesi mahakamani ili kuweza kushuhudia matumizi ya lugha katika mahakama ya Milimani, huku akirejelea malengo na maswali ya utafiti wake. Kwa hali hii basi mbinu ya kimsingi ya ukusanyaji data itahusu uchunguzi shiriki ambapo mtafiti atatazama na kunakili mambo muhimu katika mchakato wa mawasiliano baina ya mawakili na majaji. Kitabu kitatumika kama kifaa cha utafiti katika kunakili yaliyotazamwa.

Mbinu ya kurekodi na hojaji pia zitatumika katika ukusanyaji data mahakamani na baadaye data tutakayorekodi itachanganuliwa ili kubainisha jinsi vitendo usemi hutumika katika lugha ya sheria. Hili litatendeka pale ambapo unukuzi wa kila usemi mahakamani utakuwa chanagamoto kwa mtafiti. Data itakayokusanywa kwa namna hii itaweza kuandikwa kwa karatasi ili iwe sehemu ya data iliyokusanywa kwa ajili ya utafiti huu. Bali na mbinu hizi za kimsingi za ukusanyaji data tutatumia vilevile mbinu ya usomaji maktabani ili kuweza kupata yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na vilevile nadharia tutakayotumia katika uchanaganuzi wa data yetu.

### 1.9.4. MBEKO KATIKA UTAFITI

Tutapata kibali cha kushiriki kusikiliza na hata kurekodi michakato yote katika mahakama ya Milimani jijini Nairobi kutoka kwa msajili wa mahakama hiyo. kibali hiki kitakuwa cha umuhimu

ili kutuwezesha kurekodi masuala yote yanayoshughulikiwa katika mahakama. Hali hii inatokana na sababu kuwa mahakama hushughulikia masuala nyeti na mengine ya siri na hivyo data itakayorekodiwa itatumiwana mtafiti pekee.

i

### 1.9.5. UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

Data itakayokuwa imekusanywa kutoka mahakama ya Milimani, itachanganuliwa kwa mujibu wa nadharia ya vitendo usemi huku tukirejelea malengo na maswali ya utafiti katika muktadha wa sheria. Hatimaye data hii itawasilishwa kwa njia ya maelezo, mifano na mijadala. Matokeo ya utafiti kuhusu matumizi ya vitendo usemi na umuhimu wake katika sajili ya sheria itawasilishwa kwa kutumia michoro ya paichati na grafu.

### HITIMISHO

Sura hii imetoa msingi wa yale yatakayochunguzwa katika utafiti huu. Usuli wa mada, malengo ya utafiti, tatizo la utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, nadharia na mbinu za utafiti zimeelezwa kwa kina. Msingi huu utatuwezesha kuchunguza mchango wa vitendo usemi katika lugha ya sheria, huku kategoria za vitendo usemi katika lugha ya sheria zikibainishwa. Vilevile, umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria utaelezwa. Data ya utafiti huu itachanganuliwa kwa mujibu wa nadharia ya vitendo usemi. Vilevile, mchango wa nadharia hii katika utafiti huu utabainishwa. Utafiti huu pia utatoa mchango wake katika nadharia ya vitendo usemi katika kueleza mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria. Kwa kufanya hivi, utendaji wa lugha ya sheria kimazungumzo utaelezwa. Aidha, matumizi ya vitendo usemi kama mkakati wa lugha katika mawasiliano ya lugha ya sheria utaelezwa.

i

# SURA YA PILI

## 2.1. KATEGORIA ZA VITENDO USEMI KATIKA SHERIA

Sura hii inachunguza kategoria za vitendo usemi kwa kurejelea lugha ya Kiswahili na hasa vinavyotumika katika mahakama ya Milimani jijini Nairobi. Lengo kuu la sura hii ni kubainisha kategoria hizi na kuweza kuonyesha ni zipi hutumika zaidi ya zipi na kwa sababu gani. Matokeo ya sura hii yatatuwezesha kufahamu ni kategoria zipi za vitendo usemi zitumikazo zaidi katika sajili hii ya sheria hasa katika muktadha wa diskosi ya sheria, ambapo tunachukulia mahakama ya Milimani kama kielelezo cha mahakama zote nchini Kenya.

## 2.2. UCHANGANUZI WA DATA NA MIJADALA

Lugha ni kiungo muhimu katika sheria. Lugha ya sheria huwa na msamiati wa kipekee ambao huitofautisha na lugha zingine kwani msamiati ni kidokezo muhimu cha sajili yoyote ile. Kuligana na Tiersma (1999), lugha ya sheria huwa ya kiufundi. Maneno ya kiufundi ambayo huwa na maana maalum hutumika katika muktadha wa sheria. Lugha hii hutumia vitendo usemi na kwa hivyo ni lugha tendaji kwani usemi katika sheria hutekeleza jambo kutegemea msemaji

Vitendo usemi ndio msingi wa yale tutakayochunguza katika sura hii huku tukirejelea lugha ya sheria kama inavyotumika na wanasheria katika mahakama ya Milimani nchini Kenya. Utendaji wa lugha ya sheria utabainishwa kwa kuchunguza jinsi mawakili na majaji hutumia vitendo usemi kutoa kauli zao. Data kuhusu vitendo usemi itachanganuliwa kwa mujibu wa Searle (1979), ambaye aliviainisha vitendo usemi katika kategoria tano kuu ifuatavyo:

i. Vitendo elekezi
ii. Vitendo vya ahadi
iii. Vitendo vya kutaarifisha
iv. Vitendo vya uamuzi
v. Vitendo vielezi

### 2.2.1 Vitendo Elekezi

Vitendo elekezi ni vitendo ambavyo hutumia lugha kuwafanya watu watende mambo fulani. Vitendo elekezi hutumika katika kuamrisha, kushauri au kuagiza. Katika muktadha wa sheria, majaji na mawakili hutumia vitendo elekezi katika kutoa amri, kuagiza, au katika kufanya uteuzi kuhusu suala fulani la kisheria. Kwa mfano.

*Mfano wa 1 kesi ya 1.*

KM: Eleza mahakama hii majina yako kamili

SH: Jina langu ni XY___

J: Eleza majina yako kamili na kazi unayofanya

SH: Jina langu ni XYZ, nafanya kazi ya nduthi Eastleigh, yaani kazi ya boda boda

KM: Uko na kitambulisho?

SH: Niko na alien

KM: Kitambulisho iko wapi?

SH: Mimi ni refugee

*Mfano wa 2 kesi ya 1*

SH: Yeye nilikuwa na number yake, yeye na mimi sijuani sana. Alikuwa na number yangu alafu akaniuliza yeye atapata bunduki wapi hapo Mathare. Nikamwambia nitauliza rafiki yangu WT____

KM: WT anauza bunduki?

SH: Apana

KM: Mlipigiana simu na mshukiwa?

SH: Eeeh, kwa watts up lakini nilimwambia rafiki yangu WT kwamba niko na kastoma anataka

kununua bunduki Mathare

J:  Let me get this clearly…mlipigiana simu kwa watts up ama, it was watts up chatt?  WT ali

Kuwa wapi mkipigiana simu na mshukiwa?

SH:  Alinipigia simu kwa watts up

J:   KM…WT ni shahidi?

KM:  Yes your honour

J: **WT na shahidi waliobaki wafike mahakamani kesi itakaposikizwa tena.**

*Mfano wa 1 kesi ya 2*

IO: Your honour in relation to this case, I can remember very well on 31st May 2019 I received a number of exhibit as stated in the memo which was submitted to me by sergent XXX. Your honour I have a list of about forty exhibit which I wish to tender before this court. However, I will touch on the following exhibit because they are of interest to this case.

i. Mobile phone Sumsung model
ii. Safaricom sim card serial no O7________________
iii. HP laptop serial no CNU74________________

OWP: Mheshimiwa, kuhusiana na kesi hii, nakumbuka tarehe 31/5/2019 nilipokea baadhi ya uua ambazo zimetajwa katika memo niliyokabidhiwa na sagenti XXX.  Mheshimiwa nina orodha ya takribani uua arobaini ambazo ningependa kuwasilisha mbele ya maha kama hii lakini nitagusia uua zifuatazo ambazo ni za umuhimu katika kesi hii:

i. Simu ya rununu aina ya Sumsung
ii. Kadi ya simu ya Safaricom nambari 07_____________
iii. Tarakilishi aina ya HP numbari CNU74______________________

KM**: Mheshimiwa, kabla tuendelee niruhusu nitabulishe uua hizi kwa kuzipa majina:**

**Simu ya rununu exhibit MFI 9**

**Kadi ya simu ya Safaricom exhibit MFI 10**

**Tarakilishi exhibit MFI 11**

Katika maf*ano wa 1 kesi ya 1***,** kiongozi wa mashtaka pamoja na jaji wanaagiza shahidi aeleze majina yake kamili na kazi anayofanya. Shahidi anatenda kama alivyoagizwa. Katika *mfano wa2 kesi ya 1,* jaji anatoa amri kwamba WT ambaye ni shahidi katika kesi hiyo afike mahakamani pamoja na mashahidi wegine kesi itakaposikizwa tena. Katika *mfano wa 1 kesi ya 2,* kiongozi wa mashtaka anaomba jaji ruhusa ili aweze kutambulisha uua zilizowasilishwa mahakamani na ofisa wa upelelezi. Anaelekeza jaji jinsi atakavyozipa majina uua zilizowasilishwa mahakamani. Ni wazi kwamba vitendo elekezi au viagizi vinatumia lugha kuwafanya wasikilizaji kutenda jambo fulani mahakamani hapa. Kwa hivyo, vitendo hivi vinatumika katika kuelekeza ambapo msikilizaji lazima atende kama alivyoelekezwa na majaji au mawakili.

### 2.2.2 Vitendo vya Ahadi

Vitendo vya ahadi ni vitendo ambavyo hutumia lugha kutenda vitendo vya siku sijazo. Kwa mfano:

*Mfano wa 1 kesi ya 3*

KM: Je, Umekuwa miogoni mwa watu wanaotumia mihadarati?

SH: Ndio

PC: You have seen people selling narcotics, haven’t you?

W: Yes

KM: Umeona watu wakiuza mihadarati?

SH: Ndio

J: Considering that there are still other cases ready for trial, set the continuation date for this trial to be 2/11/2020.

J: **Kwa sababu kuna kesi zingine ambazo ziko tayari kusikizwa, kesi hii itasikizwa tena tarehe 2/11/2020.**

*Mfano wa 1 kesi ya 4*

PC: Do you know that lying under the oath is a crime and it is punishable? please answer the question.

W: Unajua kundaganya ni makosa unayoweza kuadhibiwa hasa ukiwa umekula kiapo? tafadhari jibu swali.

PC: Did you spend that night with Mr_________or not?

W: No

PC: Je, usiku huo mlila na Bw_____________au la?

Sh: La

PC: My lord I have no other question to this witness.

W: Mheshimiwa, sina swali lingine kwa shahidi huyu

J: After the testimony of KKK, set the cross examination of other witnesses to be on 2/11/2020

J**: Baada ya ushahidi wa KKK, udadisi wa mashahidi wengine utafanyika tarehe 27/11/2020**

*Mfano wa 2 kesi ya 3*

W: Mheshimiwa, bondi imelipwa kama ulivyoagiza. Mheshimiwa kwa sasa naomba kuachiliwa kwa pasipoti ya mshukiwa kwa sababu pasi hiyo inahitajika katika idara ya uhamiaji ili apate visa na kibali cha kufanya kazi. Haya yote yanahitajika kufanywa katika pasipoti yake ili

akubaliwe kuishi Kenya. Mheshimiwa naomba pasipoti hii iachiliwe na mahakama. Pindi tu shughuli hiyo imekamilika natairejesha pasi yenyewe mahakamani**. Naomba pia kesi hii itajwe tena tareh**e **31/10/2020.**

Katika mfano wa 1 kesi ya 3, jaji ameagiza kesi isikizwe tena tarehe 2/11/2020. Uamuzi huu unatokana na sababu kuwa, zipo kesi zingine ambazo zinahitaji kusikizwa. Katika kauli hii jaji ametumia lugha kutenda kitendo cha siku zijazo. Aidha, katika mfano wa 1 kesi ya 4, jaji ametoa amri kwamba udadisi wa mashahidi wengine katika kesi husika utafanyika katika kikao kingine mnamo tarehe 27/11/2020. Kitendo cha ahadi kinadhihirika pia katika kesi ya 3 mfano wa 2, ambapo wakili anaomba kesi itajwe tena tarehe 31/10/2020. Tumeweza kubaini kuwa wanasheria hutumia vitendo vya ahadi katika kutaja tarehe za kusikizwa kwa kesi au kutajwa kwa kesi. Vilevile, wanasheria wanaweza kutumia vitendo vya ahadi katika katika kutoa vitisho. Vitendo hivi hulazimu mtu kutumia lugha kutenda vitendo vya siku zijazo.

### 2.2.3. Vitendovya Kutaarifisha

Vitendo vya kutaarifisha ni vitendo ambavyo humfunga msemaji kwenye ukweli wa kauli fulani. Vitendo hivi humfunga msemaji katika ukweli wa yale yaliyosemwa.

*Mfano wa 2 kesi ya 1*

W: Kwa hivyo wewe ni refugee

SH: Ndio

W: Nini inaonyesha wewe ni refugee?

SH: Niko na alien

W: Hiyo alien ulipata mwaka gani?

SH: Mwaka wa elfu mbili

W: Ushawahi kaa Kakuma?

SH: La

W: Kwa hivyo mtu akisema katika mahakama hii unakaa Kakuma, atakuwa anasema ukweli au Urongo

SH: Ni urongo.

*Mfano wa 1 kesi ya 5*

PC: For how long have you known Mr ____________?

A: For a long time since we were kids

KM: Umemjua kwa muda gani Bw_______________?

SH: Kwa muda mrefu, tangu utotoni

PC: Mr________were you aware that Mr ____________was a drug trafficker and he has spent a jail term in France for trafficking drugs?

A: NO, I didn't know that

KM: Bw _______ulijua kwamba Bw_____________alikuwa mlanguzi wa dawa za kulevya na alifungwa gerezani nchini Ufaransa kwa kosa hili?

M: Apana sikujua.

Katika mfano wa 2 kesi ya 1 na mfano wa 1 kesi ya 5, vitendo usemi vya kutaarifisha vimebainika wazi kupitia kwa mazungumzo baina ya wakili na mshukiwa. Katika mazungumzo haya, msemaji ambaye ni wakili anatumia lugha ambayo hutenda vitendo vya kutaarifisha. Vitendo hivi vinamfunga msemaji katika ukweli wa yale yanayosemwa na mshukiwa. Vitendo vya kutaarifisha vilevile vimetumika katika mfano wa 1 kesi ya 4, mfano wa 1 kesi ya 1, na mfano wa 2 kesi 1. Wanasheria katika kesi hizi wamefungwa katika ukweli wa tamko fulani. Vitendo vya kutaarifisha hutumiwa na wanasheria katika kutoa mapendekezo, malalamishi au madai.

### 2.2.4 Vitendo vya Uamuzi

Vitendo vya uamuzi hujishughulisha na matamko ambayo yanabadili hali ya msikilizaji. Kufaulu kwa vitendo hivi hutegemea msemaji kwani lazima anayetekeleza kitendo kile awe na uwezo wa kufanya hivyo. Katika muktadha wa sheria, majaji ndio hutekeleza vitendo vya uamuzi.

*Mfano wa 2 kesi ya 5*

PC: Look at me in the eyes and tell me whether you have taken something today or not. Are you high or not?

KM: Niangalie na unieleze kama umevuta chochote leo. Umelewa au hujalewa?

L : Objection my lord

J : Over ruled

W : Napinga mheshimiwa

J : **Nimebatilisha**

PC : For how long have you sold drugs?

L : Objection my lord

W : Napinga mheshimiwa

J : Sustained.

J : **Nimekubaliana.**

Mfana wa 1 kesi ya 6

J: I am satistied that the prosection has proved this case against the first and second accussed persons on the respective charges facing them and therefore I find them guilty for aiding the terroriist attackers. I thefore convict them accordingly as follows ……..

J: Nimeridhika kwamba upande wa mashtaka umethibitisha kesi hii dhidi ya mshukiwa wa kwanza na wa pili kuhusu mashtaka yanayowakabili na kwa hivyo nimewapata na hatia ya kuwasaidia washambulizi wa kigaidi**. Kwa hivyo nawahukumu kuligana na makosa haya kama ifuatavyo……**

Katika kesi ya 2 mfano wa 5, jaji anatoa uamuzi baada ya wakili kupinga namna ambavyo kiongozi wa mashtaka anavyouliza mshukiwa maswali. Jaji anakubali ombi la wakili na kutoa uamuzi wake. Isitoshe, uamuzi wa jaji unadhihirika pia katika mfano wa 1 kesi ya 6. Katika kesi hii, jaji anatoa uamuzi wake kuhusiana na kesi husika inayohusu washukiwa wa kigaidi. Uamuzi huu unatokana na matumizi ya lugha ambayo yamesababisha kuhukumiwa kwa washukiwa. Kufaulu kwa vitendo vya uamuzi hutegemea msemaji kwani lazima anayetenda vitendo vile awe na uwezo wa kufanya hivyo. Katika muktadha wa sheria, vitendo hivi hutendwa na majaji kwani ndio wana uwezo wa kubadili hali ya mambo hasa kwa msikilizaji. Hali hii hutokana na uwezo waliopewa kisheria katika utendakazi wao.

**2.2.5 Vitendo vielezi**

Vitendo vielezi ni vitendo usemi ambavyo hudhihirika wakati msemaji huonyesha hali yake ya kisaikolojia. Vitendo vya aina hii hueleza hisia za msemaji. Vitendo hivi ni kama vile kupongeza, kuomba msamaha na kushukuru.

*Mfano wa 2 kesi ya 4*

J : After the testimony of KKK set the cross examination of other witnesses to be on 27/10/2020

J : Baada ya ushahidi wa KKK, udadisi wa mashahidi wengine utafanyika tarehe 27/10/2020

PC: Your honour am requesting the court to postpone the said date of cross examination to 3/11/2020 so that I can provide all the witnesses.

KM: Mheshimiwa naomba mahakama ihairishe tarehe iliyotajwa ya udadisi wa mashahidi hadi tarehe 3/11/2020 ili niweze kuleta mashahidi wote.

J : Granted

J : Ombi lako limekubaliwa

PC : Most obliged your honour

KM : **Nashukuru sana**

Katika mfano huu kiongozi wa mashtaka anashukuru mheshimiwa hakimu kwa kukubali ombi lake kuwa tarehe iliyotajwa ya kusikizwa kwa kesi ihairishwe. Vitendo usemi katika kundi hili humfanya msemaji kuonyesha hisia zake kuhusu jambo fulani. Katika utafiti wetu tumebaini kuwa vitendo hivi hutumiwa sana na washukiwa au mashahidi ikiliganishwa na wanasheria. Washukiwa na mashahidi huonyesha hisia zao kupitia ishara za uso ambazo huambatana na vilio au hata kuomba msamaha. Wanasheria, hasa mawakili, hutumia vitendo vielezi hasa wakati ambapo ombi lao kwa mahakama limekubaliwa.

## 2.3. MATOKEO YA UTAFITI KUHUSU VITENDO USEMI

Utafiti huu umeweza kubainisha kwamba lugha ya sheria hutumia vitendo usemi katika kutaarifisha, kuelekeza, kutoa uamuzi, kueleza na kutoa ahadi. Wanasheria hutumia kategoria mbalimbali za vitendo usemi katika muktadha rasmi wa kazi zao. Matumizi ya usemi ambao ni tendaji katika sheria hufanya lugha hii kuwa ya kipekee na ya kiufundi na hili ni jambo ambalo huitofautisha na lugha zingine katika jamii. Ni kutokana na matumizi ya kategoria mbalimbali za vitendo usemi ambapo tunaweza kubaini lugha ya sheria kama lugha tendaji.

Matumizi ya vitendo usemi katika sheria huifanya lugha ya sheria kuwa tata na isiyowazi kueleweka kwani usemi katika sheria hutekeleza jambo kutegemea msemaji. Utafiti huu umeweza kubaini kuwa, wanasheria hutumia vitendo usemi katika viwango tofauti tofauti. Kimatumizi, kategoria za vitendo usemi hutofautiana kwani wanasheria hutumia vitendo hivi kwa viwango tofauti. Kila kundi huhusishwa na aina fulani ya vitendo usemi ambavyo wanavitumia kuliko vingine.

Tumeweza kubaini kuwa, asilimia kubwa ya vitendo vya ahadi na uamuzi hutumiwa na majaji katika kufanikisha kazi zao kupitia vitendo usemi. Majaji hutoa maamuzi ambayo hubadilisha hali ya mambo. Jambo hili hutokana na hadhi waliyonayo kwani anayetenda vitendo hivi lazima awe na uwezo wa kufanya hivyo. Isitoshe, wanasheria hawa pia hutumia lugha kutenda vitendo vya ahadi kama vile kutaja tarehe za kusikizwa kwa kesi.

Utafiti huu umeonyesha kuwa katika mahakama ya Milimani vitendo vielekezi na vile vya kutaarifisha hutumiwa sana na mawakili. Wanasheria hawa hutumia vitendo hivi katika kuuliza maswali, kuamrisha na kutoa mapendekezo. Tumeweza kubaini kuwa vitendo usemi katika muktadha wa sheria hufanikishwa kupitia kwa maswali ambayo huulizwa na wanasheria hawa pamoja na majaji wanapokuwa wanashughulikia kesi katika mahakama ya Milimani.


Utafiti huu umebaini kuwa, vitendo vielezi kwa upande mwingine hutumiwa na wanasheria katika mahakama ya Milimani japo kwa asilimia ndogo. Vitendo hivi hutumia lugha kueleza hali za kisaikolojia za wasemaji na pia kuonyesha hisia zao. Utafiti huu umeweza kubaini kuwa asilimia kubwa ya vitendo hivi hutumiwa na washukiwa na mashahidi katika kueleza hisia zao na hali zao za kisaikojia hasa wanapojitetea katika kesi.

Tumeweza kubaini katika utafiti huu kuwa, lugha ya sheria hutumia kategoria za vitendo usemi katika viwango tofauti tofauti. Vitendo vya kutaarifisha, kuligana na utafiti huu, hutumika katika takribani mawasilano yote rasmi ya wanasheria. Vitendo hivi vinatumika zaidi na wanasheria ukilinganisha na vitendo usemi vingine kwa sababu shahidi au mshukiwa anapotoa madai huwa anatoa kauli ambazo anaamini ni za kweli au uongo na kwa hivyo vitendo hivi hutumika sana katika ufafanuzi wa mambo. Kufaulu kwa vitendo hivi hutegemea maswali ambayo huulizwa na wanasheria. Kimatumizi, vitendo vya kutaarifisha vinafuatwa na vitendo elekezi, vitendo vya ahadi, vitendo vya uamuzi na vitendo vielezi. Ufuatao ni mchoro wa pai chati unaolinganisha

matumizi tofauti ya kategoria za vitendo usemi kama tulivyochanganua data yetu. Ulinganisho huu unaonyesha frikwenzi na asilimia za matumizi ya kategoria hizi.

| **KATEGORIA ZA VITENDO USEMI** | **FRIKWENZI** | **ASILIMIA YA FRIKWENZI** |
|---|---|---|
| Vitendo vya kutaarifisha | 5 | 33 |
| Vitendo elekezi | 4 | 27 |
| Vitendo vya ahadi | 3 | 20 |
| Vitendo vya uamuzi | 2 | 13 |
| Vitendo vielezi | 1 | 7 |
| Jumla | 15 | 100 |

Haya ni matokeo ya vitendo usemi mbalimbali kama yalivyojidhihirisha kutokana na data ya utafiti wetu.




**Chanzo: Data kutokana na utafiti.**

Katika mchoro huu tumeweza kuonyesha ni vitendo vipi vinatumika zaidi na wanasheria katika mahakama ya Milimani kuliko vingine. Isitoshe mchoro huu unaonyesha asilimia za kimatumizi za kila kategoria ya vitendo usemi.

## 2.4 HITIMISHO

Vitendo usemi ni kiungo muhimu katika lugha na sheria. Matumizi ya kategoria tofauti tofauti za vitendo usemi katika Mahakama ya Milimani yamedhihirisha kwamba lugha ya sheria ni lugha tendaji. Kila usemi katika sheria huwa na utendakazi wake na kwa hivyo ni wazi kwamba sheria ni uwanja wa vitendo usemi hasa matumizi ya lugha ya sheria kimazungumzo. Utafiti huu umeweza kubaini kuwa lugha ya sheria hutumia vitendo usemi na kwa hivyo lugha hii ni lugha tendaji kwani kila usemi katika sheria hutekeleza jambo kutegemea msemaji. Vilevile, vitendo usemi mbalimbali huweza kupendelewa dhidi ya vingine katika utekelezaji wa shughuli za kisheria na wanasheria. Sura ifuatayo, itajishughulisha na suala la umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria kama ilivyojibainisha kutokana na data ya utafiti huu.

# SURA YA TATU

## 3.1. UMUHIMU WA VITENDO USEMI KWA WANASHERIA


### Utangulizi

Sura hii inalichunguza suala la umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria kwa kurejelea matukio katika mahakama ya Milimani jijini Nairobi. Sura hii inawagawa wanasheria katika matapo mawili, ambapo kuna mahakimu na mawakili. Utafiti katika sura hii utaweza kubaini kama katika hao wawili ni kundi gani linalothamini zaidi vitendo usemi katika utendakazi wake kama mkakati wa kisheria na kwa nini. Data kwa ajili ya sura hii imetokana na hojaji au kidadisi ambacho kiliwauliza maswali wanasheria hawa, lengo likiwa ni kupata maoni yao kuhusu umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria. Maswali ya hojaji yalikuwa hivi kwamba hayakuhitaji majibu ya moja kwa moja kwani yalidadisi maoni yao ya ndani. Pale ambapo mtafiti alihisi kuwa jawabu lililotolewa halikuthibitishwa kulikuwa na maswali ya ziada yaliyofuatilia ili kupata kiini hasa cha jawabu lililotolewa na watafitiwa.

## 3.2. MATOKEO YA UTAFITI KUHUSU UMUHIMU WA VITENDO USEMI KWA WANASHERIA

Katika utafiti wetu mtafiti aliweza kuwahoji wanasheria kumi na watano, ambapo alitumia hojaji kuwahoji mawakili kumi na majaji watano. Kati ya mawakili kumi waliyohojiwa, saba waliweza kujibu maswali waliyoulizwa kikamilifu. Hata hivyo, mawakili watatu kati ya hao kumi hawakujibu maswali hayo. Majaji wanne kati ya watano waliweza kujibu maswali huku mmoja akikosa kutoa jawabu lake. Matokeo ya utafiti kuhusu matapo haya mawili yamewasilishwa kwa njia ya grafu huku umuhimu wa vitendo usemi kwa makundi haya katika utendakazi wao ukielezwa kwa kurejelea mahakama ya Milimani jijini Nairobi. Kulingana na utafiti huu, vitendo usemi huwa na umuhimu kwa wanasheria wote: wawe mawakili au majaji. Kutokana na kidadisi ambacho kiliwauliza mawakili kuhusu umuhimu wa vitendo usemi katika utendakazi wao,

tuliweza kubaini umuhimu wa vitendo usemi kwa kundi hili.  Data tuliichanganua kwa mchoro wa grafu ifuatayo:





**Chanzo: Data ya utafiti**

Umuhimu wa vitendo usemi kwa mawakili umeelezwa kiasilimia kwa kulinganisha majukumu ya vitendo usemi kwa wanasheria huku tukieleza ni yepi huchangamkiwa sana na kwa nini. Majukumu haya ni: Kuhoji 57%, kuarifu 42%, kutia moyo 14%, ufafanuzi 86%, na kuamrisha 71%.  Mawakili sita walieleza kwamba vitendo usemi hutumika katika ufafanuzi wa jambo au suala fulani ili kuliweka wazi kwa manufaa ya hakimu, kiongozi wa mashtaka na hata mshukiwa.

Mawakili wapatao watano walieleza kuwa, vitendo usemi huwasaidia katika kutoa amri au kuamrisha. Vilevile, kundi hili la wanasheria lilieleza kuwa vitendo usemi huwasaidia katika kuhoji au kudadisi washukiwa na mashahidi.  Kati ya kundi hili la mawakili lililohojiwa, mawakili wanne walieleza kuwa vitendo usemi huwasaidia sana katika mahojiano. Mawakili watatu

walieleza kuwa vitendo usemi huwasaidia katika kuarifu na kutia moyo. Kutokana na uchanganuzi huu tuliweza kubaini kuwa majukumu ya vitendo usemi hutofautiana kwani kuna yale yanayochangamkiwa zaidi ya mengine. Tuliweza kubaini kuwa vitendo usemi hutumika sana na mawakili hasa katika ufafanuzi ili kuweka wazi suala fulani lieleweke vyema. Kimatumizi, jukumu hili linafuatwa na jukumu la kuamrisha, kuhoji, kuarifu na kutia moyo mtawalia kama yalivyowakilishwa kwenye mchoro wa grafu.

Majaji katika mahakama ya Milimani pia waliweza kutoa sababu zao kuhusu umuhimu wa vitendo usemi katika utendakazi wao. Kati ya majaji watano waliyohojiwa, majaji wanne waliweza kutoa sababu zao kuhusu matumizi na umuhimu wa vitendo usemi katika sheria. Hata hivyo, mmoja kati ya majaji wa kundi lililohojiwa hakutoa jawabu lake. Kulingana na majaji waliyohojiwa, vitendo usemi vina umuhimu ufuatao kisheria: kuamrisha, kutoa matangazo na kutoa ufafanuzi. Kimatumizi, majukumu haya hutofautiana kwani utafiti wetu ulibaini kuwa majaji hutumia vitendo usemi kwa wingi katika kutoa maamuzi. Jukumu hili linafuatwa na jukumu la kuamrisha na ufafanuzi mtawalia. Mchoro ufuatao wa grafu unaonyesha umuhimu wa vitendo usemi kwa majaji huku asilimia za matumizi ya majukumu ya vitendo usemi zikibainishwa:




**Chanzo: Data ya utafiti**

Kutokana na data ya utafiti wetu, majaji wanne walieleza kuwa vitendo usemi huwa vya umuhimu sana katika kutoa matangazo au maamuzi. Majaji watatu walieleza kwamba vitendo usemi hutumika katika kuamrisha huku hakimu mmoja akisema kwamba vitendo usemi huwa na jukumu la kutoa ufafanuzi hasa pale ambapo suala fulani lina utata. Kimatumizi, majukumu haya hutofautina kwani kuna yale yanayotumika zaidi ya mengine. Kuligana na data yetu majukumu haya yamewakilishwa na asilimia zifuatazo: Kutangaza 80%, Kuamrisha 60 %, na Ufafanuzi 20%. Utafiti wetu uliweza kubaini kuwa kati ya matapo haya mawili ya wanasheria, mawakili huthamini sana matumizi ya vitendo usemi katika utendakazi wao. Kundi hili hutumia vitendo usemi kama mkakati wa kufanikisha kazi zao hasa katika kuhoji, kutoa ufafanuzi, kuarifu, kuamrisha na kutia moyo wahasiriwa na waathiriwa katika kesi mahakamani. Kwa kundi hili, vitendo usemi ni mkakati wa lugha na wa kimawasiliano ambao huwasaidia hasa katika udadisi na uendeleshaji wa shughuli mbalimbali katika sheria hasa katika muktadha rasmi wa kazi zao.

## 3.3. UCHANGANUZI WA DATA NA MIJADALA KUHUSU UMUHIMU WA VITENDO USEMI

### 3.3.1 Kuamrisha

Vitendo usemi hutumika katika kutoa amri. Tuliweza kubaini kuwa amri inaweza kutoka kwa wakili au jaji. Kwa mfano:

***Mfano 3.1***

KM: Unafanya kazi gani?

SH: Kazi ya boda….

KM: **Ongea kwa sauti!**

Umesema unafanya kazi gani?

***Mfano 3.2***

KH: Alikupigia simu ama alikuchat?

SH: Alipiga watts up.

J: Sisi tunataka kujua ukweli ili hii korti ifanye haki kwa__________

J: **Wacha kutupotezea wakati**

**Stop making our lives difficult, sema ukweli unaojua.**

***Mfano 3.3***

W: Did yo know that_______________ was having a pistol that night? **Yes, or No?**

Unajua kwamba ______________ alikuwa na bunduki usiku huo? **Ndio au La?**

SH: La

Katika mifano wa 3.1, kiongozi wa mashtaka anaamrisha shahidi aongee kwa sauti ya juu ili asikike. Katika mfano wa pili 3.2, jaji anaamrisha shahidi atoe ushahidi wa kweli na kuweka bayana masuala anayoulizwa ili aweze kuelekeza mahakama katika maamuzi kuhusu suala husika. Katika mfano wa 3.3, wakili anauliza shahidi maswali ambayo anataka atoe jibu la ndio au la. Kusudi lake lilikuwa kuelekeza shahidi katika jinsi ya kujibu maswali ili asije akatoa maelezo mapana yasiyohitajika. Ni wazi kwamba vitendo usemi huwa na umuhimu kwa mawakili na majaji kwani makundi haya hutumia amri mbalimbali kutoa mwongozo na maelezo kwa mashahidi au washukiwa. Aidha, kwa kutoa amri, wanasheria hawa huzuia ushahidi wa uongo kutolewa mahakamani.

### 3.3.2 Kutoa ufafanuzi

Mawakili na majaji hutumia vitendo usemi katika ufafanuzi wa masuala tofauti katika muktadha wa kazi zao. Ufafanuzi huu hufanikishwa kwa njia ya maswali ambayo huulizwa na wanasheria hawa ili kuweza kuweka wazi mambo yanayoweza kuwa na utata fulani. Vilevile, vitendo usemi huwa vya umuhimu kwa makundi haya hasa katika kubainisha dhana ambazo zinaweza kuwa na utata fulani kusudi ziweze kueleweka. Kwa mfano:

***Mfano 3.4.***

W: **Kwa hii statement kuna mahali umeandika one hour? Angalia vizuri.**

SH: Apana.

W: **Kwa hii statement kuna mahali uliandikisha jina_______________?**

SH: Apana

W: **Kwa hivyo, baada ya kuandikisha statement ndio uliskia kuna jina kama __________?**

*Mfano3.5*

KM: My lord, the 4th name on that list should be of interest to this court. It is that of Mr ___

yet he claims that he was not in___________ at that particular day.

**Mheshimiwa, jina la nne katika orodha hii lina mvuto kwa mhakama hii, kwani ni jina**

**La___________ambaye anadai kuwa hakuwa katika___________siku hiyo.**

*Mfano 3.6*

KM: Your honour, before we continue, to avoid confusion the said exhibit is dated 27/8/2019 and therefore, I wish you have the same marked as MF1 8.

**Mheshimiwa kabla tuendelee, uua unaorejelewa ni wa tarehe 27/8/2019 na kwa**

**Hivyo ningependelea utambulishwe kama MF1 8 ili kuondoa utata.**

*Mfano 3.7*

KM: _____________anauza bunduki?

SH: Apana yeye hajauza

SH: Ama tuongee Amharic

J: If he is comfortable, am going to record that he has chosen to speak Amharic

Any objection council_________________?

**Kama ameridhika, nitanakili kuwa amechagua kuzungumza kwa lugha ya Amharick.**

**Wakili______________ unapingamizi lolote?**

Katika mfano wa 3.4, wakili anatoa ufafanuzi kwa korti kwa njia ya maswali kwa shahidi kwamba, katika taarifa iliyotolewa na shahidi hakunakili jina la mshukiwa. Katika muktadha huu wakili anajaribu kuonyesha kuwa ushahidi unaotolewa ni wa uongo. Katika mfano wa 3.5, wakili anafafanua kuwa jina la mshukiwa liko katika orodha ya majina ambayo yamewasilishwa mahakamani kama ushahidi. Katika mfano wa 3.6, kiongozi wa mashtaka anatoa ufafanuzi kuhusu uua uliyowasilishwa mahakamani na kuelekeza jaji jinsi ushahidi huo utatambulishwa. Shabaha ya wakili huyu ni kuondoa utata kuhusiana na suala husika. Katika mfano wa 3.7, jaji anafafanua kuwa atanakili kuwa shahidi ameomba kutumia lugha ya Kiamhari ambayo anaielewa vyema kuliko lugha ya Kiswahili.

### 3.3.3 Kuhoji

Vitendo usemi huwa na umuhimu sana katika mahojiano. Mawakili hutumia vitendo usemi katika kuhoji washukiwa na hata mashahidi. Umuhimu huu hufanikishwa kwa njia ya maswali ambayo yanaweza kuwa ya kijumla, maswali ya ndio au la, au maswali yanayohusiana na masula husika. Maswali huwa ni mkakati wa kimawasiliano ambao hutumiwa ili kuwezesha ujenzi wa kesi katika misingi ya maelezo yaliyowasilishwa. Kwa mfano:

***Mfano 3.8***

W: Kwa hivyo wewe ni refugee?

SH: Ndio

W: Nini inaonyesha wewe ni refugee?

SH: Niko na alien

W: Hiyo alien ulipata mwaka gani?

SH: Mwaka wa elfu mbili

W: Ushawahi kaa Kakuma?

SH: La

***Mfano3.9***

W:  Bwana _____________--

SH: Ndio, kwa nini unatoa ushahidi wa uongo?

W: Wakati uliandikisha statement mlikuwa na_______________?

Katika mifano hii, wakili anauliza maswali kwa njia ya kuwahoji mashahidi. Kusudi la maswali haya ni kufanya mashahidi kutoa ufafanuzi kuhusu ushahidi wanaowasilisha. Aidha, wakili anatumia maswali ya ndio au la kama njia ya kumfunga msemaji asije akatoa ufafanuzi wa kina kuhusu suala husika. Kwa kufanya hivi, majibu huwa yamekitwa katika swali lenyewe na kwa hivyo matumizi ya vitendo usemi hasa maswali ya ndio au la huweza kuwa na athari hasi kwa shahidi au hata mshukiwa ambaye huenda asitoe ushahidi wake kwa uwazi.

### 3.3.4 Kutia moyo

Data ya utafiti huu imebaini kuwa vitendo usemi hutumiwa na wanasheria katika kutia moyo na hili huonekana hasa kutoka kwa kiongozi wa mashtaka kwa shahidi kama njia ya kuonyesha shahidi kwamba ushahidi anaoutoa ni mzuri na kwamba aendelee vivyo hivyo.  Kwa mfano:

***Mfano 3.10***

KM: Tafadhali, tunataka kujua ukweli, kwa hivyo utaongea Kiswahili, mambo ya Amharic

hatutaki tena.

Alikwambia nini kwa hiyo simu?

SH:  Aliniambia yeye anataka nimpeleke yeye____________

KM:  **Endelea …, tunaendelea vizuri, hiyo Kiswahili broken unaongea vizuri.**

### 3.3.5 Kuarifu

Vitendo usemi hutumika pia na wanasheria katika kuarifu au kutaarifisha. Mawakili hutumia vitendo hivi kuarifu mahakama kuhusu suala fulani hasa jambo ambalo linahitajika maelezo fulani.

***Mfano 3.11***

J: That should be exhibit 2?

Huo ni uua wa pili?

KM: Yes my lord, it is a video showing how young men get recruited to terrorism and the training they undergo.

**Naam mheshimiwa. Hii ni video inayoonyesha jinsi vijana huingizwa katika ugaidi na mafunzo ambayo wao hupitia.**

Katika mfano wa 3.11, jaji anauliza kiongozi wa mashtaka swali kuhusu uua uliyowasilishwa mbele ya mahakama. Kiongozi wa mashtaka anafafanua zaidi na kutaarifisha mahakama kuhusu uua huo, kwamba ni video inayoonyesha jinsi vijana huingizwa katika ugaidi, na mafunzo ambayo vijana hao hupitia. Kitendo cha kutaarifisha kinadhihirika kupitia mazungumzo baina ya wakili na jaji. Jaji katika muktadha huu amefungwa katika ukweli wa kauli zinazotolewa na kiongozi wa mashtaka katika kutaarifisha mahakama kuhusu uua aliyowasilisha.

### 3.3.6 Kutangaza

Kutokana na data ya utafiti huu, ni wazi kuwa majaji hutumia vitendo usemi katika kutoa matangazo. Hali hii hutokana na hadhi yao kisheria na kwa hivyo kwa kutumia vitendo usemi wao huweza kutangaza na kutoa uamuzi kuhusu jambo fulani. Kwa mfano:

***Mfano 3.12***

KM: Umeona watu wakiuza mihadarati?

SH: Ndio

J: Considering that there are still other cases ready for trial, set the continuation date for this trial to be 2/11/2020.

J: **Kwa sababu kuna kesi zingine ambazo ziko tayari kusikizwa, kesi hii itasikizwa tena tarehe 2/11/2020.**

***Mfano 3.13.***

PC: My lord, I have no other question to this witness.

W: Mheshimiwa, sina swali lingine kwa shahidi huyu

J: After the testimony of KKK, set the cross examination of other witnesses to be on 2/11/2020

J**: Baada ya ushahidi wa KKK, udadisi wa mashahidi wengine utafanyika tarehe 27/11/2020**

## 3.4. HITIMISHO

Baada ya kupitia kile ambacho tunaona kuwa ni umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria, tunahitimisha sura hii kwa kutoa kauli hizi zinazofuata na ambazo zimetokana na data ya utafiti huu. Katika utafiti huu tumeweza kubaini kuwa mawakili hutumia vitendo usemi kwa wingi ikilinganishwa na majaji. Kundi hili hutumia vitendo usemi katika takribani mchakato wote wa mawasiliano katika muktadha rasmi wa utendakazi wao. Hali hii huweza kufanya vitendo usemi kuwa vya umuhimu zaidi kwa kundi hili, ambapo wao hutumia vitendo hivi katika kutoa ufafanuzi, kutaarifisha, kutia moyo, kuamrisha na kuhoji.  Kwa upande mwingine, majaji hutumia vitendo usemi katika kutoa matangazo, kutoa ufafanuzi na kuamrisha.  Utafiti huu umebaini kuwa vitendo usemi ni mkakati wa lugha ambao hutumiwa na wanasheria katika kufaulisha kazi zao za uanasheria.  Hata hivyo, matumizi ya vitendo hivi huweza kuwa na athari hasi kwa makundi mengine yanayohusika katika kesi kwani wao huwa hawana uelewa wa lugha kama ilivyo kwa wanasheria. Katika sura ifuatayo, tumechunguza mchango wa vitendo usemi kama mkakati wa kimawasiliano kwa sajili ya sheria.

# SURA YA NNE

## 4.1. MCHANGO WA VITENDO USEMI KWA SAJILI YA SHERIA

### UTANGULIZI

Sajili ni lugha si kutegemea mtumizi bali matumizi. Hoja hii ina maana kuwa, kila sajili huwa na sura zake pamoja na sifa ambazo ni za kipekee. Yaani, mtu yule mmoja atatumia lugha iliyo na sifa za kipekee kutegemea sajili husika. Sura hii inatathmini mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria ili kutofautisha vitendo usemi katika sajili zingine zile. Data kwa ajili ya sura hii imetokana na mbinu za utafiti ambazo zimehusisha uchunguzi shiriki kwa upande wa mtafiti na vilevile hojaji kwa upande wa wanasheria.

## 4.2. MATOKEO KUHUSU UMUHIMU WA VITENDO USEMI KATIKA SHERIA

Katika sehemu hii ya sura ya nne, tutachunguza umuhimu wa vitendo usemi katika sheria kwa njia ya mjadala. Kwa hali hii basi, umuhimu wa vitendo usemi katika sheria waweza kuwa chanya au hasi.

Danet (1980), anasema kuwa sheria haingekuwepo bila uwepo wa lugha. Lugha ni muhimu sana katika utekelezaji wa sheria. Matumizi ya lugha katika muktadha wa sheria yanaweza kusababisha athari chanya au hasi kutegemea matumizi yake. Wanasheria hutumia lugha kwa namna ya kipekee na hili ni jambo ambalo huwatofautisha na makundi mengine ya kijamii. Lugha ya wanasheria katika muktadha wa kazi zao husheheni matumizi ya vitendo usemi. Matumizi ya vitendo usemi katika sheria huwa na umuhimu ufuatao kama ulivyobainika kutokana na utafiti wetu. Mifano tutakayotoa ili kutilia nguvu vitendo usemi katika sajili hii ya sheria inatokana na tafsiri yetu ya yale yaliyosemwa na wahojiwa ambao ni wanasheria katika utendakazi wao.

### 4.2.1 Uchunguzi au udadisi

Wanasheria hutumia vitendo usemi katika uchunguzi au udadisi wa mashahidi. Katika muktadha wa sheria vitendo usemi hutumika katika mahakama ambapo wanasheria hutekeleza kazi zao. Katika muktadha wa mahakama, wanasheria hasa mawakili hutumia vitendo usemi kama mkakati wa lugha ambao huwasaidia kufanikisha kazi zao. Mawakili, hutumia vitendo usemi katika kuchunguza au kudadisi mashahidi. Vitendo usemi hutumika na kundi hili katika kuamrisha, kuonya, kuhoji, na katika kutoa fafanuzi mbalimbali. Kwa kufanya hivi sauti ya mawakili husikika sana katika mchakato wote wa mawasiliano mahakamani. Hali hii hutokana na kutaka kujua ubora na uthabiti wa kesi wanazoshughulikia. Shabaha nyingine ni kuwa, wanasheria hutaka kujua ukweli wa yale yanayotolewa kama ushahidi mbele ya hakimu. Katika udadisi wa mashahidi, matumizi ya kategoria mbalimbali za vitendo usemi hudhihirika hasa kupitia maswali ambayo huulizwa mashahidi. Vitendo vya kutaarifisha na viagizi hubainika katika mawasiliano ya mawakili. Katika mchakato wa mawasiliano haya, majaji pia huonekana wakitumia kategoria za vitendo usemi hasa vitendo vya ahadi na vitendo vya uamuzi. Matumizi ya vitendo usemi kwa mawakili kama mkakati wa lugha huweza kuathiri walengwa hasa mashahidi ambao hutumia lugha ya kawaida na hawana uelewa wa vitendo usemi kama ilivyo kwa mawakili. Hali hii huwa na athari hasi kwa mashahidi. Isitoshe, uamuzi wa mahakama hutolewa kuligana na maelezo yaliyowasilishwa na kwa hivyo matumizi ya lugha kwa wanasheria huenda yakatoa mwelekeo fulani ambao husababisha uamuzi ambao hutolewa na hakimu. Ifuatayo ni mifano ya baadhi ya vitendo usemi vilivyotumika na mawakili katika uchunguzi au udadisi wa mashahidi.

***Vitendo usemi vya kuhoji***

L: Did the detective tell you that your brother took a pistol and pointed it to XXXX.

W: **Je, ofisa wa upelelezi alikujuvya kuwa ndugu yako alielekeza bunduki kwa XXXX**?

W:  Did you know that?  Yes, or NO.

W: **Ulijua hivyo?  Ndio au la.**

L: Did the detective inform you that your brother used the pistol to hit XXXX and gave him a black out. Did he tell you that? Yes, or NO.

W: **Je, ofisa wa upelelezi alikueleza kuwa ndugu yako alifiatua bunduki kwa XXXX hadi akazirai? Ndio au la.**

L: Objection my lord, this is actually an abuse of the witness. The witness is being asked repeated questions and he is not given an opportunity to answer the questions.

W: Napinga mheshimiwa, hii ni dhuluma kwa shahidi. Shahidi anaulizwa maswali mfululizo bila kupewa nafasi ya kujibu maswali hayo.

***Vitendo usemi vya kutoa ufafanuzi***

L: May lord am applying for bail of my client based on self recognition.

W: Mheshimiwa, naomba dhamana kwa mteja wangu kuligana na ninavyomfahamu.

J: Self recognition?

J: Unavyomfahamu?

L: Yes, may lord, my client Mr YYY is a reputable gentleman, someone who in his entire life has never been to the police station for any matter of crime. He is a businessman who I can describe not capable of killing someone.

W: **Ndio mheshimiwa, bwana YYY ni mteja wangu anayeheshimika. Ni mtu ambaye katika maisha yake hajawahi kuwa katika kituo cha police kwa sababu ya uhalifu wowote. Ni mwanabiashara ambaye naweza kueleza kuwa hawezi kumuua yeyote.**

J:  We are not yet on trial council.

J:  Wakili, bado hatujanza kesi.

L:  Am aware my lord, am only clarifying my plea my lord, that bail be granted to my client.

W:  **Najua mheshimiwa, nafafanua tu ombi langu kwamba, mteja wangu apewe dhamana.**

***Vitendo usemi vya kuamrisha***

***Mfano wa 1***

PC:  Now Mr KKK you said you were not at that hotel on the very day you murdered your Wife?

KM:  Bwana KKK ulisema haukuwa katika hoteli hiyo siku ambayo ulimuua mke wako?

L:  Objection my lord that question is most suggestive.

W:  Napinga mheshimiwa, swali hilo linapendekeza sana.

J:   Sustained, prosecuting council you should know better than anyone else how to ask such questions.

J**:  Nakubaliana, kiongozi wa mashtaka unapaswa kufahamu zaidi ya mtu mwingine yeyote jinsi ya kuuliza maswali ya aina hiyo**.

PC:     Am sorry my lord.

***Mfano wa 2***

J:  **Wacha kutapatapa na kutupotezea wakati. Na ujue wakili wa XXX yuko hapa atakuuliza maswali. Sisi tunataka kujua ukweli, ili mahakama hii ifanye haki kwa**

___________**Sema ukweli.**

KM: Tafadhali tunataka kujua ukweli, hii case is very serious, kwa hivyo utaongea Kiswahili.

Mambo ya Amharick hatutaki tena.

### 4.2.2 Kudhibiti mahusiano ya watu katika jamii

Sheria ina jukumu la kimsingi la kuongoza tabia za watu na kudhibiti mahusiano yao katika jamii. Sheria haiundwi au kutumika katika ombwe tupu katika jamii yoyote ile. Mifumo ya kisheria ni njia mojawapo ambayo huonyesha uhai wa jamii, kwani sheria huwa na lengo mahususi la kuongoza jamii katika mwelekeo fulani. Ukiukaji wa sheria husababisha adhabu fulani kwa waliyokiuka. Hali hii hudhihirika kupitia ufafanuzi wa sheria kupitia mfumo wa mahakama. Vitendo usemi hutumika katika ufafanuzi wa sheria kupitia mahakama. Wanasheria hutumia vitendo usemi katika muktadha wa mahakama ili kufanikisha jukumu la sheria la kudhibiti mahusiano ya watu katika jamii. Kwa kufanya hivi, haki hupatikana. Majaji na mawakili hutumia vitendo usemi katika diskosi ya sheria kama kichocheo katika mchakato wa kuleta mabadiliko katika jamii. Mabadiliko haya hutokana na jinsi lugha imetumika na wanasheria katika mchakato wa kesi mahakamani.

Majaji hutumia vitendo usemi vya uamuzi katika kuhakikisha haki imepatikana kwa walengwa katika kesi zilizowasilishwa mbele yao. Sheria hutumia lugha kimaandishi na kimazungumzo katika kudhibiti mahusiano ya watu katika jamii na kwa hivyo sheria haingekuwepo bila uwepo wa lugha. Lugha ya sheria kimaandishi huhusishwa na katiba ambayo hutoa mwelekeo na mwongozo kwa wanajamii. Aidha, utendakazi wa wanasheria hutegemea lugha ya sheria kimazungumzo katika kutoa fafanuzi, mielekeo na maamuzi katika diskosi ya sheria. Kwa hali hii basi matumizi ya vitendo usemi, hasa na wanasheria ni mojawapo ya sifa zinazobainisha sajili ya sheria. Wanasheria hutumia kategoria mbali mbali za vitendo usemi kama vile vitendo elekezi, vitendo vya ahadi, vitendo vya kutaarifisha na vitendo vya uamuzi.

**Vitendo elekezi**

***Mfano wa 1***

Vitendo elekezi ni vitendo ambavyo hutumia lugha kuwafanya watu watende mambo fulani. Vitendo elekezi hutumika katika kuamrisha, kushauri, au kuagiza. Kwa mfano:

L: Am aware my lord, am only clarifying my plea my lord, that bail be granted to my client.

W: Najua mheshimiwa, natoa ufafanuzi wa ombi langu, kwamba mteja wangu apewe dhamana.

PC: My lord this is a criminal case of murder.

KM: Mheshimiwa, hii ni kesi ya mauaji.

J: Exactly, on the strength of that, bail is denied. The suspect is to be remaded in prison Custody. The case is adjourned until 30th of September 2020.

J**: Kweli, kwa sababu hii, mshukiwa hatapewa dhamana. Atawekwa kwenye rumande. Kesi hii imehairishwa hadi tarehe 17/9/ 2020.**

***Mfano wa 2***

PC: Mr KKK, on that day your wife died, please tell this court where you were?

KM: Bwana KKK, eleza mahakama hii ulikuwa wapi siku ambayo mke wako alikufa.

AP: I was in Nairobi.

M: Nilikuwa Nairobi.

PC: In Nairobi?

KM: Nairobi?

PC: In your house?

KM: Nyumbani?

AP: No

M: Apana

PC: So where were you?

KM: Kwa hivyo, ulikuwa wapi?

AP: In a hotel.

KM: Katika hoteli?

AP: Yes, I needed to rest, to have some private moment with myself.

***Mfano wa 3***

W: Kwa hivyo mtu akisema katika mahakama hii unakaa Kakuma, atakuwa anasema ukweli au Urongo.

SH: Ni urongo

W: Unamjua _______?

SH: Simjui.

W: Unajua biashara anayofanya __________?

SH: Siijui.

**W: Umeapa kuwa utasema ukweli, unajua ni kosa kuongea urongo ukiwa tayari umechukua kiapo katika mahakama?**

**SH: Ndio**

**W:  Kwa hivyo ongea ukweli, umeapa kuwa utasema ukweli**.

Katika mfano wa kwanza, jaji anatoa amri kwamba mshukiwa hatapewa dhamana na mahakama kwa sababu kesi yake inahusu mauaji. Vilevile, hakimu anatoa amri kwamba mshukiwa awekwe kwenye rumande hadi kesi itakaposikizwa tena tarehe 17/9/2020.  Katika mfano wa pili, kiongozi wa mashtaka anaelekeza mshukiwa katika kujibu maswali ambayo ndio msingi wa udadidi wa kesi husika. Mshukiwa anajibu maswali kama alivyoelekezwa na kiongozi wa mashtaka. Katika mfano wa 3, wakili anamshauri shahidi ajibu maswali bila kudanganya mbele ya mahakama. Kiongozi wa mashtaka anamshauri mshukiwa aseme ukweli kwani ni hatia kudanganya mahakama hasa baada ya kula kiapo. Ni wazi kwamba vitendo elekezi vinatumia lugha kumfanya msikilizaji kutenda jambo fulani mahakamani kama alivyoelekezwa na hakimu au wakili.

***Vitendo vya ahadi***

Vitendo vya ahadi ni vitendo ambavyo hutumia lugha kutenda vitendo vya siku zijazo. Kwa mfano:

***Mfano wa 1***

L:   My lord we are talking of a criminal case of murder.

J:  Exactly, on the strength of that, bail is denied. The suspect is to be remaded in prison Custody.  The case is adjourned until $30^{th}$ of September 2020.

J: Kweli, kwa sababu hii, mshukiwa hatapewa dhamana. Atawekwa kwenye rumande**.  Kesi hii imehairishwa hadi tarehe 17/9/ 2020.**

***Mfano wa 2***

KK: Majina yako kamili?

SH: XYZ

KK: Wewe ni wa dini gani?

SH: Mimi ni mkristu

KK: Inua bibilia hii na urudie maneno haya.

SH**: (akiinuabibilia na kula kiapo) mimi XYZ, naapa ya kwamba, maneno ambayo nitasema kwa hii koti ni ukweli mtupu. Eee mungu nisaidie.**

Katika mfano wa kwanza jaji anatenda kitendo cha ahadi kwa kuahirisha kesi hadi tarehe 17/9/2020. Mifano wa pili unahusu kitendo cha ahadi ambacho hufanyika katika mahakama japo kitendo cha aina hii hakihusiani moja kwa moja na mawakili au majaji. Shahidi anakula kiapo na kuahidi kwamba maneno atakayoyasema mahakamani ni ukweli mtupu.

***Vitendo vya uamuzi***

Vitendo vya uamuzi hujishughulisha na matamko ambayo hubadili hali ya msikilizaji. Anayekitenda kitendo cha uamuzi, lazima awe na uwezo wa kufanya hivyo. Kwa mfano:

L: My lord we are talking of a criminal case of murder.

J: Exactly, on the strength of that, bail is denied. The suspect is to be remaded in prison Custody. The case is adjourned until $30^{th}$ of September 2020.

J: **Kweli, kwa sababu hii, mshukiwa hatapewa dhamana. Atawekwa kwenye rumande. Kesi hii imehairishwa hadi tarehe 17/9/ 2020.**

Katika mfano huu, hakimu anakataa ombi la wakili la kumpa mshukiwa dhamana. Hakimu anatoa uamuzi mshukiwa awekwe kwenye rumande hadi kesi itakaposikizwa tena tarehe 12/9/2020. Kwa kufanya hivi hakimu ametenda kitendo cha uamuzi.

***Vitendo vya kutaarifisha***

Vitendo vya kutaarifisha humfunga msemaji kwenye ukweli wa kauli fulani. Vitendo hivi humfunga msemaji katika ukweli wa yale yaliyosemwa. Kwa mfano:

PC: Can you please state your name for the record.

KM: Tafadhali eleza majina yako kamili.

AP: My name is ___________

M: Jina langu ni____________

PC: Are you employed?

AP: Yes, am the manger of XYZ company.

KM: Umeajiliwa?

M: Ndio, mimi ni meneja wa kampuni ya XYZ

PC: How long have you been in that position?

AP: Two years

Katika mfano huu, vitendo vya kutaarifisha vimebainika wazi kupitia mazungumzo kati ya kiongozi wa mashtaka na mshukiwa. Kauli za mshukiwa zinamfunga wakili katika ukweli wa yale yaliyosemwa na mshukiwa. Matumizi ya vitendo usemi vya ahadi, uamuzi, vitendo elekezi na vitendo vya kutaarifisha katika diskosi ya sheria vinadhihirisha kuwa, sajili ya sheria hutumia vitendo usemi.

### 4.2.3 Uamuzi wa mahakama

Maamuzi ya mahakama huhusisha mchakato wa sentensi ambazo huwa tekelezi au tendaji. Uamuzi huu hutolewa na majaji ambao wana uwezo huo kisheria. Uamuzi wa mahakama huwa ni

matokeo ya mchakato wa kesi mahakamani. Maamuzi ya mahakama huhusisha ukweli na umantiki kuhusu kesi husika. Katika sura ya pili, tulibaini kuwa lugha ya wanasheria husheheni matumizi ya vitendo usemi vya kutaarifisha, vitendo vielezi, vitendo elekezi, vitendo vya ahadi na vitendo vya uamuzi. Majaji hutumia vitendo vya uamuzi katika kutoa hukumu. Hali hii huweza kubadilisha hali ya mambo kwa walengwa katika kesi. Uamuzi huu huweza kuwa na athari chanya au hasi kwa walengwa hawa. Athari hizi hutokana na jinsi mawakili walivyotumia lugha hasa vitendo usemi kama mkakati wa kipragmatiki katika kudadisi washukiwa au mashahidi.

Lugha ya mawakili huchangia sana katika matokeo ya kesi kwani majaji hufanya uamuzi kuli ngana na yale yaliyowasilishwa mbele yao. Hali hii hufanya lugha ya sheria kuwa tendaji kwani kila tamko katika lugha ya sheria hutenda jambo. Utendaji wa lugha ya sheria hubainika katika kuelekeza, kutoa ahadi, kuagiza na kutoa hukumu. Wanasheria hutumia kategoria mbalimbali za vitendo usemi katika muktadha wa sheria. Lugha katika sheria huwa tendaji ukilinganisha na sajili zingine zile. Asilimia kubwa ya maneno ambayo hutumika katika sheria huwa na jukumu kisheria. Hali hii hufanya lugha katika sajili ya sheria kuwa tekelezi. Kwa mfano:

***Mfano***

J: The court is going to sentence Mr_______ as follows:

With regard to count no 1, murder in the first degree as it is related to ________, the court is going to sentence you a life sentence that could run consequtively with count number 3. With regard to count number 4 and 5 as it relates to tampering with the deceased body, the court is going to impose a maximum imprisonment of ten years that will run consequitively with other counts.

J: Mahakama itamhukumu Bwana __________ ifuatavyo.

Kuligana na shtaka la kwanza kuhusu mauaji ya ____________, mahakama itakuhukumu kifungo cha maisha ambacho kitaenda sambaba na shtaka la pili na la tatu. Kuligana na shtaka la nne na

la tano linalohusiana na uharibifu wa mwili wa marehemu, mahakama itakuhukumu kifungo cha miaka kumi ambacho kitaenda sabamba na vifungo vingine.

Majaji hutumia lugha tekelezi katika kutoa uamuzi wao. Jambo hili hutokana na uwezo waliyopewa kisheria. Maamuzi yao huweza kubadili hali ya mambo. Hali hii hufanya lugha ya wanasheria kuwa tendaji na ya kuamrisha kwani lazima walengwa wafuate amri au agizo lililotolewa na mahakama kupitia kwa majaji.

### 4.2.4 Kuhoji na kutoa ufafanuzi

Vitendo usemi, hasa vitendo vya ilokusheni, hutumika sana katika diskosi ya sheria. Wanasheria hutumia vitendo hivi katika kutoa amri na ufafanuzi kuhusu masuala wanayoshughulikia. Kwa mfano.

P: Mr _____________ on 25th /08/2015 at 10:30 PM, you went to XXXX hotel with a gun and shot ____________who was your legally married wife. Guilty or not guilty.

KM: Bwana _____________ Mnamo tarehe 25/08/2015 saa 10.30 usiku, ulienda katika hoteli ya XXXX na kumpiga risasi____________ ambaye alikuwa mke wako halali kisheria. Una hatia au huna?

A: Not guilty.

M: Sina hatia

P: My lord may I also tender this in evidence.

KM: Mheshimiwa naomba kuwasilisha ushahidi huu

J: That should be exhibit two?

J: Huo ni uua wa pili

P: Yes, my lord, it is the list of lodgers at XXXX hotel one week before and one week after the date in question. My lord the 20th name and of interest to this court is that of Mr_________

KM: Ndio mheshimiwa, ni orodha ya wageni waliolala katika hoteli XXXX wiki moja kabla na

Baada ya tukio hili. Mheshimiwa, jina nambari ishirini ni la umuhimu kwa mahakama hii

Kwani ni jina la bwana _______________

Katika mfano huu kiongozi wa mashtaka anahoji mshukiwa na kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu suala analolishughulikia katika kesi husika. Anatoa ushahidi kwa hakimu ili kuweka wazi yale anayoeleza. Katika sura ya tatu tulibaini kuwa mawakili hutumia vitendo usemi katika kuamrisha hasa, wakati ambao wanataka shahidi atoe ushahidi wa kweli. Kundi hili la wanasheria vilevile, hutumia vitendo usemi katika kutoa fafanuzi kuhusu masula ambayo huleta utata ili kuyaweka wazi. Kwa mfano:

W: Kwa hivyo mwenye kuandika hii statement ni mrongo? (akimpelekea statement na kuagiza

Karani wa koti aisome)

W: Katika hiyo statement kuna mahali umeandika jina _____________

SH: Apana, niliandika XXX, jina __________nimesikia leo

W: Kwa hivyo, baada ya kuandika statement ndio umeskia jina _________? Wewe ni mrongo,

na usitupotezee wakati hapa.

Majaji kwa upande mwingine huweza kuhoji walengwa katika kesi hasa wakati ambao wanataka kupata ukweli na uwazi kuhusu suala fulani. Wanasheria hawa hutumia vitendo usemi vya kutaarifisha na elekezi ili kufanikisha kazi zao. Kwa mfano:

J: Let me get this clearly......, mlipigiana simu kwa watts up ama it was a watt up chatt. WT

alikuwa wapi mkipigiana simu na mshukiwa?

SH: Alinipigia simu kwa watts up

J: KM……WT ni shahidi?

KM: Yes your honour

J: **WT na shahidi waliobaki wafike mahakamani kesi itakaposikizwa tena.**

Matumizi ya vitendo usemi kwa wanasheria katika lugha ya sheria ni kigezo muhimu katika utambuzi wa kundi hili la kijamii. Upekee katika matumizi ya lugha ya wanasheria huwatambulisha kama kundi la kijamii. Lugha yao kimazungumzo huwa na sarufi na msamiati maalum hasa katika muktadha wa kazi zao. Matumizi ya vitendo usemi kwa wanasheria hufanya lugha ya sheria kutofautiana na lugha zingine kimsamiati. Kwa mfano:

***Mfano wa 1***

P: What happened to your Christianity? are you not a Christian?

KM: Ni nini kilifanyika kwa ukristo wako? Je, wewe si ni mkristo?

L: Objection my lord, we are not talking about Christianity here.

W: Napinga **mheshimiwa**, hatuzungumzi kuhusu ukristo.

P: My lord, am cross examining, that where **my learned friend** Mr _________ is going wrong.

Am placing an evidence before this honourable court.

KM: Mheshimiwa, nafanya udadisi, jambo ambalo **rafiki na msomi mwenzangu** Mr__________

anakosa kuelewa. Natoa ushahidi wangu mbele ya mahakama hii.

J: Objection overruled, please proceed with the questions.

J: Nimebatilisha, naomba uendelee na udadisi wako.

***Mfano wa 2***

The court is going to sentence the accussed as follows: the 1$^{st}$ and 4$^{th}$ accussed person on count no 2 charge of conspiracy to commit terrorist act contrary to section 23 and 4 of the prevention of terrorism act. The 1$^{st}$ and 4$^{th}$ accussed person on count 3 and 12 respectfully for knowingly supporting terrorism act contrarly to section 9 of the prevention of terrorism act.

Mahakama itawahukumu washukiwa ifuatavyo: Mshukiwa wa kwanza na wa nne kwa mashtaka ya pili kuhusu njama ya kutenda ugaidi kinyume na sheria kifungu cha ishirini na tatu na kifungu cha nne kuhusu kuzuia vitendo vya ugaidi. Vilevile, mshukiwa wa kwanza na wa nne watahukumiwa kwa mashtaka ya tatu na ya kumi na mbili mtawalia kwa kuunga mkono vitendo vya kigaidi ambavyo ni kinyume na sheria kifungu cha tisa kuhusu uzuiliaji wa vitendo vya kigaidi.

Katika mifano hii, wanasheria wametumia misamiati maalum kama vile mheshimiwa, rafiki yangu msomi na marejeleo ya vifungu vya kisheria. Misamiati hii ni kitambulisho cha kundi hili la kijamii hasa, wanapoitumia katika mazingira ya kazi zao. Hali hii hufanya lugha ya sheria kuwa changamano ukiliganisha na lugha zingine kama vile lugha ya michezoni na lugha ya biashara. Wanasheria vilevile, hutumia sentensi ndefu ndefu ambazo huwa na maelezo marefu na ya undani. Matumizi ya sentensi ndefu ndefu hufafanua na kuweka wazi kinachozungumziwa kisheria. Kwa mfano:

*J***:** *Nimeridhika kwamba, upande wa mashtaka umethibitisha kesi hii dhidi ya mshukiwa wa kwanza na wa nne kuhusu mashtaka yanayowakabili, na kwa hivyo nimewapata na hatia ya kuwasaidia washabulizi wa kigaidi. Kwa hivyo, nawahukumu kuligana na makosa haya kama ifuatavyo: Mshukiwa wa kwanza na wa nne kwa mashtaka ya pili kuhusu njama ya kutenda ugaidi kinyume na sheria kifungu cha ishirini na tatu na kifungu cha nne kuhusu kuzuia vitendo vya ugaidi. Vilevile, mshukiwa wa kwanza na wa nne watahukumiwa kwa mashtaka ya tatu na ya kumi na mbili mtawalia kwa kuunga mkono vitendo vya kigaidi ambavyo ni kinyume na sheria kifungu cha tisa kuhusu uzuiliaji wa vitendo vya kigaidi***.**

Mawakili vilevile, hutumia maelezo marefu hasa wanapotaka kuweka wazi masuala tata kuhusu wanayoshughulikia. Majaji pia hutumia maelezo marefu hasa wanapotoa hukumu. Hali hii husababishwa na haja ya kutaka kutoa hukumu iliyojengeka katika misingi ya ukweli na uwazi. Kwa kufanya hivi, vitendo usemi huwa ndio msingi wa maelezo ya wanasheria hawa kwani kila usemi katika sheria huwa na jukumu tendaji.

Vitendo usemi katika sheria hutumika katika kuhoji na kutoa ufafanuzi. Haya hudhihirika kwa njia ya maswali ambayo hutumika katika mahojiano ambayo hufanyika mahakamani. Wanasheria hutumia maswali kama njia ya kupata ukweli na uwazi kuhusu yanayochunguzwa. Maswali haya

huwa ni msingi wa baadhi ya vitendo usemi ambavyo hutumika na wanasheria. Jambo hili hufanya lugha katika sajili ya sheria kuwa lugha yenye udadisi mwingi hasa inapotumika na wanasheria.

Kwa mfano:

KM: Unaweza kumbuka number ya YYY, alipochukua number yako ya simu, wewe na yeye mliongea nini?

SH: Aliniambia yeye anataka bunduki

KM: Alikupigia saa ngapi?

SH: Saa nne usiku

KM: Alikwambia nini kwa hiyo simu?

SH: Aliniambia wewe unaingia mathare, nataka bunduki

KM: Kwani wewe unauza bunduki na kwa nini yeye anakwambia yeye anataka kununua bunduki?

SH: Apana siuzi bunduki

Majaji na mawakili hutumia maswali kama mkakati wa kufanya udadisi na kuweka wazi masuala mbalimbali wanayochunguza.

### 4.2.5. Kutaarifisha au kuarifu

Bix (1996), anasema kwamba lugha ni chombo ambacho ni muhimu katika utekelezaji wa sheria. Umuhimu wa lugha katika sheria hubainika wazi kimaandishi na kimazungumzo kwa sababu ya majukumu yake. Lugha sio tu chombo cha kufahamu sheria bali ni njia ya kuitambua sheria. Wanasheria hutumia lugha kimazungumzo katika kutaarifisha. Vitendo usemi vya kutaarifisha hutumika na mawakili katika kutoa mapendekezo, malalamishi au katika kutoa madai. Katika sura ya pili tulibaini kuwa vitendo usemi vya kutaarifisha ndio hutumika kwa wingi katika diskosi ya sheria. Vitendo hivi hutumika katika takribani mchakato wote wa kesi mahakamani. Vitendo vya kutaarifisha ni vitendo ambavyo humfunga msemaji kwenye ukweli wa kauli fulani. Vitendo hivi

humfunga msemaji katika ukweli wa yale yaliyosemwa. Mawakili na majaji hutumia vitendo vya vya kutaarifisha kupitia mazungumzo baina yao na washukiwa au mashahidi. Kwa mfano:

***Mfano wa 1***

KM: Tafadhali, tunataka kujua ukweli. Hii case is very serious kwa hivyo, utaongea Kiswahili mambo ya Amharic hatutaki tena hapa

KM: Mlipopatana Garrisa lodge na YYY, kulifanyika aje?

SH: YYY alichukua number yangu. Nikambeba kutoka section 1 hadi mathare.

KM: Mliongea kwa simu?

SH: Eeeh

KM: Kupitia number gani? Patia koti hiyo number

SH: 072______________

***Mfano wa 2***

KM: Kwa hivyo wewe na _____________mlienda kwa polisi?

SH: Eeeh tukapata ofisa anaitwa ____________alafu huyo ofisa akanipea polisi tatu akaniambia mimi nipigie mshukiwa. Tulitoka na polisi hadi section 1 at Oromo mosque

KM: Mlipofika hapo mlipigia YYY?

SH: Tulimpigia

KM: YYY Anaishi wapi?

SH: Section one

KM: Alichukua muda gani kufika.

SH: Hakukaa

Katika mfano wa kwanza na wa pili vitendo vya kutaarifisha vimebainika kupitia mazungumzo baina ya kiongozi wa mashtaka na shahidi. Katika mazungumzo haya msemaji ambaye ni kiongozi wa mashtaka anatumia lugha ambayo hutenda vitendo vya kutaarifisha. Vitendo hivi vinamfunga msemaji katika ukweli wa yale yanayosemwa na shahidi.

Lugha ya sheria hutumia maneno ya kawaida ambayo maana yake si ya kawaida, yaani maneno haya huwa na maana ya kisheria. Katika kutaarifisha lugha ya kawaida huweza ikatumika lakini maana yake huweza kuwa tofauti kisheria. Hali hii hutokana na hoja kuwa kila tamko la kisheria huwa na jukumu lake. Kwa sababu hii, lugha ya sheria si wazi na kwa hivyo ni vigumu kwa mtu wa kwaida kuielewa. Utata huu unaweza kusababisha athari hasi kwa walengwa katika kesi hasa kutokana na kutoelewa maana ya matumizi ya lugha kisheria. Kwa mfano:

L: You are telling us all this to entertain us. Arent you? You are simply wasting court time.

W: Unasema haya yote ili utufurahishe, sivyo? Unapotezea mahakama hii wakati.

S: No, no….am not making anything up.

M: Hapana, hapana……sindanganyi chochote.

L: Very well, please tell me, how did Mr___________know that you are able to do this job?

W: Vizuri sana, naomba ueleze jinsi Bwana __________alijua kwamba unawezafanya kazi hii?

S: Because Mr_____ knew me, so he recommended me.

M: Kwa sababu Bwana___________alinijua na kwa hivyo alinipendekeza nifanye kazi hii.

L: So Mr________ the convicted drug trafficker knew you.

W: Kwa hivyo Bwana_________aliyehukumiwa kama mlanguzi wa dawa za kulevya alikufahamu?

S: Yes, he knew me.

M: Ndio, alinifahamu.

L: Are you a professional drug smuggler?

W: Je, wewe ni mlanguzi wa dawa za kulevya?

S:( As he stands up and starts talking using gesture) No, No, No……. that not true at all. As I said earlier, am a port master, may be you don't have such a job in Kenya, but in my home country there is. (he starts crying), may be the interpreter is not able to interprete what am saying, that why you are not understanding. You don't seem to understand what kind of people I was dealing with. And now am being accused of something I didn't do.

*M:(Akisimama na kuanza kuzungumza kwa ishara) hapana, hapana, hapana……hiyo si kweli kabisa. Kama nilivyosema awali, mimi ni mkuu wa bandari, pengine hamna kazi kama hiyo nchini Kenya, lakini katiki nchi yangu kazi hiyo ipo. (anaanza kulia), pengine mkalimani hawezi kutafsiri yale ninayosema, ndio maana hamnielewi. Inaonekana hauelewi aina ya watu niliyohusiana nao. Na sasa natuhumiwa kwa kosa ambalo sikufanya.*

L: Thankyou your honour, that complete my cross examination.

W: Asante mheshimiwa, nimemaliza udadisi wangu.

Katika mfano huu, wakili anaendeleza udadisi wake kwa mshukiwa ili aweze kutaarifisha na kuweka wazi masuala ambayo alitaka yaeleweke na mahakama. Udadisi huu unaendelezwa kwa njia ya maswali, ambapo wakili anamhoji mshukiwa ili apate ukweli kuhusu kesi husika. Kwa upande wake, mshukiwa anaonekana kutoridhika na jinsi maswali hayo yanavyoendelezwa na kuona kwamba wakili haelewi ushahidi ambao mshukiwa anautoa mbele ya mahakama. Maswali haya yanaendelezwa kwa lugha ya kawaida lakini maana ya maswali haya si wazi, kwani mshukiwa anaweza akajifunga katika kauli anazozitoa mbele ya mahakama, jambo ambalo linaweza kusababisha yeye kuhukumiwa kutokana na ukweli wa yale aliyoeleza mbele ya mahakama.

## 4.3. HITIMISHO

Katika sura hii tumechunguza na kutahmini mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria. Utafiti wetu umeweza kubaini kuwa, lugha katika sajili ya sheria huwa tendaji ukiliganisha na sajili zingine zote. Utendaji wa lugha katika sajili ya sheria hutokana na matumizi ya vitendo usemi kwani kila tamko katika sheria huwa na utendakazi wake. Utafiti huu umebaini kuwa vitendo vya ilokusheni hutumika katika lugha ya sheria katika kategoria tofauti. Vitendo hivi hutumika katika kutoa uamuzi, kutaarisha, kuhoji, kuelekeza na kuagiza. Matumizi ya vitendo hivi huwa na athari chanya kwa asilimia kubwa ukiliganisha na athari hasi. Kauli hii inatokana na ukweli kuwa wanasheria hutumia vitendo usemi katika diskosi ya sheria ili kupata ukweli na uwazi kuhusu masuala wanayochunguza. Wanasheria hutumia lugha tendaji katika utendakazi wao, jambo ambalo hufanya lugha ya sheria kuwa tekelezi, na kwa hivyo kuitofautisha sajili ya sheria na sajili zingine zote. Utendakazi wa lugha katika sajili ya sheria unadhihirisha kuwa sajili ni lugha si kutegemea mtumizi bali matumizi.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAHITIMISHO, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO

## 5.1. UTANGULIZI

Utafiti wetu kuhusu vitendo usemi umekamilika. Katika sura hii tutahitimisha kazi yetu kwa kutoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, mahitimisho, changamoto na mapendekezo kwa tafiti za baadaye kuhusu vitendo usemi katika sajili ya sheria. Shabaha ya utafiti huu ilikuwa ni kuchanganua lugha katika sajili ya sheria. Utafiti wetu kuhusu lugha ya sheria umeegemea mtazamo wa kipragmatiki, lengo letu hasa likiwa kuchunguza upekee wa lugha katika sajili ya sheria.

## 5.2. MUHTASARI

Sajili ya sheria imedhihirisha uwepo wa matumizi ya vitendo usemi. Katika sura ya pili tumechunguza kategoria za vitendo usemi katika lugha ya sheria. Utafiti wetu umebaini kuwa kategoria mbalimbali za vitendo usemi hutumiwa na wanasheria katika diskosi ya sheria. Vitendo usemi hutumiwa na kundi hili la kijamii katika muktadha rasmi wa mazungumzo yao. Mawakili na majaji hutumia vitendo usemi vya kategoria mbalimbali katika mawasiliano yao huku kila kundi likihusishwa na matumizi ya kategoria hizi kwa wingi kuliko lingine. Tumebaini kuwa vitendo vya kutaarifisha, vitendo vya ahadi, uamuzi na vielezi hutumika. Kategoria hizi hutofautiana kimatumizi kwani kuna vile vinavyotumika kwa wingi kuliko vingine. Vitendo vya kutaarifisha hutumika kwa asilimia kubwa na wanasheria huku vikifuatwa na vitendo elekezi, ahadi, uamuzi na vitendo vielezi mtawalia. Matumizi ya vitendo usemi kwa makundi haya hufanya lugha ya sheria kuwa tekelezi kwani kila usemi katika sheria una jukumu lake. Matumizi ya vitendo usemi yamedhihirisha kuwa nadharia ya vitendo usemi inaakisi sajili ya sheria.

Katika sura ya tatu tulichunguza suala la umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria. Mahakimu na mawakili walihojiwa ili kuweza kubaini ni kundi gani linalothamini vitendo usemi kati ya matapo haya mawili. Kutokana na utafiti wetu tuliweza kubaini kuwa vitendo usemi huwa na umuhimu kwa wanasheria hawa kwani mawakili hutumia vitendo usemi katika kuamrisha, kutoa

ufafanuzi, kuarifu, na kuhoji. Asilimia kubwa ya mawakili hutumia vitendo usemi katika kuhoji. Haya hufanyika ili kuweka wazi masuala wanayochunguza. Mahakimu pia hutumia vitendo usemi katika kuamrisha, kutoa matangazo na kutoa ufafanuzi. Kwa majaji, asilimia kubwa ya vitendo usemi hutumika katika kutoa maelezo. Kwa makundi haya, vitendo usemi huwa na umuhimu katika kazi yao kwani vinatumika kama mkakati wa lugha, ambao huwasaidia katika utekelezaji wa kazi zao kisheria.

Katika sura ya nne tulichunguza mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria. Tulibaini kuwa vitendo usemi huwa na mchango mkubwa katika lugha ya sheria kwani takribani mawasiliano yote ya wanasheria ambayo hufanyika katika sheria, hasa muktadha wa mahakama hutawaliwa na matumizi ya vitendo usemi. Wanasheria hutumia vitendo usemi kama mkakati wa mawasiliano yao. Matumizi ya vitendo usemi huweza kuwa na athari chanya au hasi. Kwa wanasheria vitendo usemi huwa na athari chanya kwani wao hutumia vitendo usemi kama mkakati wa lugha katika kudadisi, kutaarifisha, kutoa ufafanuzi na kutoa maamuzi. Hata hivyo, vitendo usemi huweza pia kuwa na athari hasi kwa walengwa. Kwa mfano, uamuzi wa hakimu unaweza kubadili hali ya mambo ya mtu binafsi hasa jaji anapotoa hukumu kisheria. Utafiti huu kuhusu matumizi ya vitendo usemi katika sheria umedhihirisha kwamba lugha ya sheria ni lugha tendaji. Hali hii inadhihirisha kuwa sajili ni lugha si kutegemea mtumizi bali matumizi.

## 5.3. MAHITIMISHO

Katika tasnifu hii tumeonyesha jinsi lugha ya sheria ni lugha tendaji. Nadharia ya vitendo usemi imetumika katika uchanganuzi wa lugha ya sheria kimazungumzo. Katika kufanya hivi tuliongozwa na malengo matatu:

i. Kuonyesha kategoria za vitendo usemi katika sajili ya sheria katika muktadha wa Kiswahili

ii. Kubainisha umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria

iii. Kutathmini mchango wa vitendo usemi katika sajili ya sheria

Utafiti tuliyofanya umebaini kuwa kategoria tano za vitendo usemi ambazo ni vitendo vya uamuzi, ahadi, elekezi, viagizi na vitendo vya kutaarifisha hutumika katika diskosi ya sheria. Kategoria hizi hutofautiana kimatumizi. Matumizi ya vitendo usemi katika sheria hufanya lugha ya sheria kuwa lugha tendaji. Kwa kurejelea mifano mbali mbali, tumedhihirisha jinsi kila usemi katika lugha ya sheria huwa na jukumu lake.

Lengo letu la pili lilikuwa ni kubainisha umuhimu wa vitendo usemi kwa wanasheria. Tumebainisha kuwa wanasheria hutumia vitendo usemi kama mkakati wa lugha kisheria. Tumeonyesha jinsi mahakimu na mawakili hutumia vitendo usemi na vilevile umuhimu wa vitendo hivi kwa makundi haya. Vitendo usemi hivi ni kama vifuatavyo:

i. Vitendo vya uamuzi
ii. Vitendo vya ahadi
iii. Vitendo elekezi
iv. Vitendo vya kutaarifisha
v. Vitendo viagizi

Tumetahmini mchango wa vitendo usemi kwa sajili ya sheria. Katika utafiti wetu tumebaini kuwa matumizi ya vitendo usemi katika sheria huwa na athari hasi na chanya kwa watumizi na walengwa. Vilevile, tumeweza kudhihirisha kuwa sajili ni matumizi ya lugha si kutegemea mtumizi bali matumizi. Mhusika mmoja anaweza kubadili lugha yake kutegemea masiala ya kijamii kama vile muktadha anamojikuta, kazi anayoifanya au lengo lake la kimawasiliano.

## 5.4. CHANGAMOTO ZA UTAFITI.

Katika utafiti wetu tumekubana na changamoto kadhaa. Haikuwa rahisi kukusanya data katika mahakama ya Milimani kwani si kila wakati ambapo kesi zilisikizwa, nyakati zingine kesi zilihairishwa kutokana na ukosefu wa ushahidi au ombi kutoka kwa mawakili.

Haikuwa rahisi kupata kibali cha kufanya utafiti baada ya mlipuko wa ugonjwa wa uviko 19 kwani shughuli za mahakama zilisitishwa kwa muda, ilitubidi kufuata maagizo tuliyopewa ya kungoja hadi wakati shughuli za mahakama ziliporejelea kama kawaida. Wakati mwingine kesi ziliendelezwa kupitia mtandao jambo ambalo liliathiri ukusanyaji wa data hivyo basi utafiti huu umechukua muda mwingi kuliko ulivyokusudiwa.

## 5.5. MAPENDEKEZO

Utafiti wetu ulibanwa na upeo na mipaka ambayo tulinuia kutafitia. Tulijikita katika nadharia ya vitendo usemi ambayo imetumika kama msingi wa utafiti wetu kuhusu sajili ya sheria. Data ya utafiti huu imechanganuliwa kwa mujibu wa nadharia hii. Tungependekeza watafiti wa baadaye wachunguze sajili ya sheria kwa kutumia mitazamo mingine ya kipragmatiki kama vile nadharia ya upole ya uso iliyoasisiwa na Penalope Brown[i] na Levinson Brown. Hii itawezesha kupata uelewa wa jinsi matumizi ya vitendo usemi katika diskosi ya sheria huathiri uso hasi na uso chanya wa binadamu.

Utafiti wetu ulifanyika katika mahakama ya Milimani ambayo tuliteua kama kiwakilishi cha mahakama nyingine. Tungependekeza utafiti ufanywe katika zaidi ya mahakama moja zinazotofautiana kihadhi ili kuweza kuakisi hali halisi ya sajili ya sheria kwa upande wa vitendo usemi na kuliganisha matokeo hayo.

Diskosi ya sheria ni pana mno, hatukuweza kujishughulisha na masuala yote yanashughulikiwa na sheria hasa kupitia mfumo wa mahakama. Utafiti wetu ulijikita katika kitengo cha mahakama kinachojishughulisha na kesi za jinai. Tungependekeza wasomi wa baadaye wafanye utafiti ambao utachunguza vitengo vingine bali na hiki tulichokishughulikia.

**MAREJELEO**


Austin, J. (1962), *How to do things with words*. Oxford university Press: London.

Bix. B. (1996*), law, language, and legal determinancy*. Clarendon press. Oxford.

Cotterill, J. (2002), *Language in the Legal process*: Palgrave Macmillan .UK.

Danet, B. (1980), *Language in the Legal Process:* Law and Society Review. Imekomolewa kutoka http://www.jstor.org/stable/3053192.

Eades, D. (2000). *I don't think it's an answer to the question: Silencing Aboriginal Witness in* Court. Language in Language: Cambridge University Press. Cambridge.

Fairclough, N. (1989), *Language and Power*: Longman.London.

Kiguru, G. (2014*). A Critical Discourse Analysis of Language used in Selected Courts of Law inKenya*. Tasnifu ya uzamivu (Haijachapishwa). Chuo kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Kothari C.R. (2004). *Research Methodology:* Methods and techniques. New Age International Publishers. New Delhi.

Lyons, (1977). *Semantics, Vols. 1 and 2*: Cambridge University Press. Cambridge

Mugenda, A. (2008). *Social Science Research: Theory and Principles*. Applied Research and Training Services. Nairobi

Pride, J. B. (1971), The *Social Meaning ofLanguage*: Oxford University Press. Newyork

Searle (1979), *Expression and Meaning: Studies in the Theory of Speech Acts*: Cambridge University Press. Newyork.

Tiersma, P. M. (1999). *Legal Language*. University of Chicago Press.

Trudgill, P. (2000), Social linguistics: *An Introduction to Language and Society*: Penguin Books, London.

Waithera, N. (2014*), Changamoto za Kutafsiri Matini za Kisheria: Tathmini ya Katiba ya Kenya* (*2010).* Tasnifu ya uzamili. (Haijachapishwa): Chuo kikuu cha Nairobi.

Wambui, G. (2015), *Sajili ya Matangazo ya Biashara Mtazamo wa Kipragmatiki*. Tasnifu ya uzamili (haijachapishwa): Chuo kikuu cha Nairobi.

Wardhaugh, R. (2002), *An Introduction to Sociolİnguistics*: Blackwell Publishing. Oxford.

Wood, S. (2012), *Courtroom Discourse as a Verbal Performance: Describing the Unique SocialLinguistic Situation of the American Trial Courtroom.*Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa), Brighan Young University.

Woodbury, H. (1984), *The Strategic Use of Questions in Court:* Semiotica.

## DATA YA UCHANGANUZI

Sehemu hii inahusu data ambayo tulikusanya katika mahakama ya Milimani, data hii ni kiwakilishi cha data ambayo tulikusanya kwa ujumla katika utafiti wetu. Data hii imehifadhiwa katika hali yake halisi bila kufanyiwa mabadiliko yoyote.

KM: Eleza mahakama hii majina yako kamili

SH: Naitwa XY

KM: Uko na kitambulisho

SH: Niko na Alien

KM: Imeandikwa jina gani

SH: Imeandikwa XYZ

KM: Uko na miaka mingapi

SH: Eighteen

KM: Unafanya kazi gani

SH: Kazi ya nduthi yaani Bodaboda

KM: Wapi

SH: Easleigh section 1

KM: Unakumbuka tarehe 5/8/2019

SH: Yes

KM: Nini kilifanyika

SH: Hiyo siku mimi nimebeba mteja kuelekea Garrisa lodge

KM: Unajua jina lake

SH: Eeeh

KM: Anaitwa nani

SH: Anaitwa YYYY

KM: Unamjua yeye

SH: Eeeh kama kastoma yangu

KM: Ulikuwa unamjua mbeleni

SH: Eeeh, yeye anakuja kama kastoma nabeba yeye, sijui sana yeye

KM: Ulikuwa umembeba mara ngapi

SH: Mara mingi

KM: Sasa vile ulimbeba nini ilifanyika

SH: Yeye aliniambia, nataka kununua bunduki

J: Ati alisema nini?

SH: Anataka kununua bunduki

J: Yeye ndiye alitaka bunduki

SH: Yeye, mimi najua anaishi Easleigh section 1 na aliniambia anataka bunduki hapo mathare

J: Na alikwambia anataka bunduki mathare

SH: Yeye alitaka bunduki nikaambia rafiki yangu WT kuna kastoma anataka bunduki.

KM: Unauza bunduki wewe

SH: Apana

KM: Kwa nini alikwambia anataka kununua bunduki?

KM: Unakuanga na number yake ya simu

SH: Yeye nilikuwa na number yake, yeye na mimi sijuani sana, alichukua number yangu, alafu akaniuliza yeye nanunua bunduki wapi, nikamwambia nitauliza rafiki yangu WT

KM: WT anauza bunduki

SH: Apana

KM: Did you contact the accussed.

SH: Yes, but I shared with my friend WTthe information about my customer who want to buy a gun

J: Let me get this clearly were they chating or it was a call, and where was WT when you were communicating with the accussed.

KM: Was it a watt up call or a chat?

SH: Alinipigia simu

J: Wacha kutapatapa na kutupotezea wakati. Na ujue wakili wa accussed yuko hapa atakuuliza maswali.

J: KM is WT a witness in this case

KM: Yes, your honour

J: WT should be presented in court during the next hearing

J: Sisi tunataka kujua ukweli ili hii koti ifanye haki kwa YYYY

KM: Tafadhali tunataka kujua ukweli hii case is very serious, kwa hivyo utaongea Kiswahili mambo ya Amharic hatutaki tena hapa

KM: Mlipopatana Garrisa lodge na YYYY, kulifanyika aje?

SH: YYYY alichukua number yangu. Nikambeba kutoka section 1 hadi mathare.

KM: Mliongea kwa simu?

SH: Eeeh

KM: Kupitia number gani? Patia koti hiyo number

SH: 072_____________

KM: Unaweza kumbuka number ya YYYYY, alipochukua number yako ya simu, wewe nay eye mliongea nini.

SH: Aliniambia yeye anataka bunduki

KM: Alikupigia saa ngapi

SH: Saa nne usiku

KM: Alikwambia nini kwa hiyo simu

SH: Aliniambia wewe unaingia mathare, nataka bunduki

KM: Kwani wewe unauza bunduki na kwa nini yeye anakwambia yeye anataka kununua bunduki

SH: Apana siuzi bunduki

KM: Mlipongea watts up, mliongea nini?

SH: Mimi nilimwambia YYYY tuweke sauti, yeye anatumia mimi na mimi natumia yeye.

KM: Mlitumiana nini

SH: Yeye alinitumia picha ya bunduki tatu

KM: YYYY Alikutumia picha ya bunduki, akakwambia anataka hiyo bunduki

SH: Yeye anasema mimi nitakupatia pesa mingi tafutia mimi hiyo bunduki

KM: Ulitafuta

SH: Apana

SH: Tulienda kwa polisi station pangani mimi na rafiki yangu

KM: Kwa hivyo wewe na ____________mlienda kwa polisi.?

SH: Eeeh tukapata ofisa anaitwa ___________alafu huyo ofisa akanipea polisi tatu akaniambia mimi nipigie mshukiwa. Tulitoka na polisi hadi section 1 at Oromo mosque

KM: Mlipofika hapo mlipigia YYYY?

SH: Tulimpigia

KM: YYYY Anaishi wapi?

SH: Section one

KM: Alichukua muda gani kufika.

SH: Hakukaa

J: Sasa wakili wa YYYY atakuuliza maswali

W: Umeeleza mahakama hii jina lako ni nani?

SH: XXXXX

W: Wewe ni mwananchi wa wapi?

SH: Ethiopia

W: Tueleze ni vipi wewe ni mwananchi wa Ethiopia na saa hii unaishi Eastleigh

W: Nini ilikuleta Kenya

SH: Mimi nimetoka Ethiopia hadi Kakuma 2000

W: Kwa hivyo wewe ni refugee

SH: Eeeh

W: Nini inaonyesha wewe ni refugee

SH: Niko na Alien

W: Hiyo Alien ulipata mwaka gani?

SH: 2019

W: Na ulikuja Kenya 2000?

W: Ushawahi ishi Kakuma?

SH: Apana

W: Kwa hivyo mtu akiambia hii mahakama ulitolewa Kakuma, ukaletwa hapa Nairobi ili utoe ushahidi, huyo mtu atakuwa mlongo?

SH: Ni kweli

W: Kwa hivyo mimi nikisema unakaa Kakuma ni ukweli au ni ulongo?

SH: ni ulongo

W: Unajua YYYY

SH: Simjui

W: Unajua biashara ambayo YYYY alikuwa anafanya?

SH: Sijui

W: Umeapa kuwa utasema ukweli?

W: Unamjua YYYYama humjui?

W: YYYYY alikuwa anafanya biashara gani?

SH: Kuuza miraa

W: Ni siku gani ulijua YYYYanishi wapi

SH: Yeye najua ni customer

W: Umesema ulipeleka polisi kwa YYYY, unajua nyumba yake ama hujui.

SH: Sijui nyumba yake najua tu anaishi section 1

W: Yaani mahali anaishi unajua lakini nyumba yake hujui. Ulijuaje anaishi section 1?

W: Kwa hivyo unajua mahali ma customer wako wote huuishi?

SH: Apana

W: Lakini unajua anishi section 1 stage

SH: Eeeh

W: Hauna habari YYYY-alifanya kazi ya kuuza miraa

SH: Mimi sijui kazi yake anafanya

W: Kuligana na ushahidi wako unasema ulipata cutomer ukamdrop Garissa lodge

SH: Eeeh

W: Alafu baada ya kumdrop kulifanyika nini?

W: Wacha nikusomee ulivyoandika kwa statement

Ulipigiwa simu uende ATPU kutoka anti terrorism police unit, lakini hukuenda hiyo siku. Simu ulipigiwa tarehe 20/8/2019.

SH: Apana

W: Umelazimishwa kutoa ushahidi

SH: NO

W: Hili ni jina lako?

SH: (akitazama) Eeeh, ni jina langu.

W: Ni wewe uliandika hii statement?

SH: Eeh ni mimi

W: Kwa hivyo unadanganya hii mahakama?

SH: Apana

W: Kwa hivyo wewe ni mlongo

SH: Apana

W: Baada ya YYYY kuomba number yako, mliongea for how long?

SH: One hour

W: Kwa hivyo hii korti irecord one hour

SH: Apana

W: Kwa hivyo unadanganya

SH: Apana

W: Ulizungumza na yeye baada ya masaa mangapi

SH: One hour

W: Kwa hiyo statement uliyosomewa kuna mahali umeandika one hour?

SH: No

W: Kwa hivyo wewe ni mlongo

SH: Apana

W: Kwa hivyo mwenye kuandika hii statement ndiye mlongo

W: Kwa hii statement kuna mahali umeandika YYYY

SH: Apana niliandika Omar nimejua jina YYYY leo

W: Kwa hivyo baada ya kuandika statement ndio umejua jina YYYY

SH: Eeeh

W: Mheshimiwa sina swali lingine kwa huyu shahidi,

# VIAMBATISHO

## QUESTIONAIRE ON USE OF SPEECH ACT BY JUDGES AND LAWYERS AT MILIMANI LAW COURT

Dear respondent.

In our effort to conduct research on use of speech act in the context of law at milimani law court, we invite you to participate in this research. The research intends to survey the use of speech act by judges and lawyers. Your participation in this research project is voluntary. Your responses will be confidential and the data from this research will only be used for academic purpose.

Thankyou in advance for your feedback.

| | |
|---|---|
| **Name** | |
| **Email** | |
| **Gender** | ○ Male<br>○ Female |
| **Prefession** | ○ Judge<br>○ Lawyer |
| **Experience** | ○ 1-3 yrs<br>○ 3-5 yrs<br>○ 5 -10 yrs<br>○ > 10 yrs |

**Please answer the following questions**

1. How important is the use of speech acts to your profession as a judge/ a lawyer?
    - ○ Not important
    - ○ Important
    - ○ You have no idea

2. How often do you use the speech acts?

- o Most of the time
- o Some of the time
- o Never

3. What is the importance of the use of speech act to judges and lawyers?

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **989311**

Date of Issue: **24/July/2021**

# RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Miss.. LUCY NJOKI GATUNE of University of Nairobi, has been licensed to conduct research in Nairobi on the topic: SAJILI YA SHERIA MTAZAMO WA VITENDO USEMI for the period ending : 24/July/2022.**

License No: **NACOSTI/P/21/11951**

**989311**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commision for Science, Technology and Innovation -